Jumamosi Februari 24, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581596

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US



**ALONSO HANA JIBU KUHUSU LIVERPOOL, BAYERN MUNICH**

UKURASA 22



**Msafara** Naibu Waziri Mkuu wapata ajali tena

UKURASA 4

**Mahakama** yafuta kesi adhabu ya kukiri kosa

UKURASA 2

**Wataalam** afya waonya hatari ya kulala na jiko la mkaa

UKURASA 5

MIAKA 7 YA KESI

# Kilichombeba mjane wa Bilionea Msuya kuachiwa

• **HUKUMU** yasomwa kwa saa nane, dakika sita, Jaji akaa mwanzo mwisho... *Endelea Ukurasa 3*



Baadhi ya ndugu, jamaa na marafiki wakifurahia nje ya Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam jana, baada ya mahakama hiyo kuwaachia huru mjane wa aliyekuwa mfanyabiashara wa madini, Erasto Msuya, marufu kama Bilionea Msuya, Miriam Mrita na mwenzake, Revocatus Muyella 'Ray'. **Picha ndogo**, Mrita na Muyella wakiwa kizimbani wakati hukumu dhidi yao ikisomwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Askari polisi auawa vurugu mgodini

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 24

### SIMBA YAANZA KUUNDA KIKOSI CHA MSIMU UJAO

WAKATI kukiwa na taarifa ya kutaka kumchukua mshambuliaji Fiston Mayele kwa mkopo kutoka Pyramids ya Misri, Uongozi wa Simba umeanza mchakato wa kukitengeneza kikosi imara cha msimu ujao kwa kuwinda wachezaji kadhaa wa ndani na nje ya nchi...

# Msako magari yenye ving'ora, 'vimulimuli' waja

UKURASA 2

**MICHEZO** **GAMONDI: NI MECHI MUHIMU KUSHINDA** UK.24

**MAONI** UK.6



Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda (mbele kulia), akikagua maendeleo ya ujenzi wa jengo la ofisi ya mkuu wa wilaya ya Butiama, alipofanya ziara ya kikazi wilayani humo mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Askari polisi auawa vurugu mgodini

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

VURUGU zinazodaiwa kutokea katika mgodi wa dhahabu unaomilikiwa na kampuni ya Shanta, Ikungi mkoani Singida, baada ya kuvamiwa na zaidi ya wananchi 50, zimesababisha kifo cha askari polisi, Konstebo James Msesi.

Askari huyo anadaiwa kufariki dunia baada ya kupigwa risasi na mwenzake wakati akiwatawanya wananchi hao waliokuwa na silaha za jadi, waliovamia kibanda chao mgodini hapo.

Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Thomas Apson, alithibitisha jana kutokea kwa tukio hilo huku akisema kundi la wananchi hao lilivamia kibanda cha askari hao juzi usiku wakiwa na silaha za jadi, ikiwamo mikuki.

"Mcheki RPC (Kamanda wa Polisi Mkoa) mchana atakuwa na taarifa kamili za tukio maana alikesha wilayani kwangu kwa ajili ya kushughulikia tukio hilo," alisema Apson, akibainisha kuwa uchunguzi wa tukio hilo unaendelea.

Meneja Mkuu wa mgodi huo, George Kondela, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo lililotokea juzi saa 5:00 usiku mgodini hapo katika kijiji cha Sambaru, Kata ya Mang'onyi na kusisitiza kuwa maelezo zaidi yatatolewa na Jeshi la Polisi mkoani Singida.

"Hili ni tukio la kihalifu na tukio lolote la kihalifu lazima liripotiwe kwenye vyombo vya ulinzi na usalama. Ninakushauri ufike katika ofisi ya RPC au kwa OCD Ikungi (Mkuu wa Polisi wa Wilaya) limesharipotiwa huko kwao na wao ndio wanaopaswa kutolea maelezo ya tukio hilo," alisema.

Kamishna wa Madini Mkoa wa Singida, Sabai Nyansiri, alipoulizwa alikiri kutokea kwa tukio hilo na kusema amezipata kutoka kwa Meneja Mkuu wa Mgodi wa Shanta.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Stella Mutabihirwa, alipofuatwa na gazeti hili eneo la makazi ya nyumba za askari polisi, Mtaa wa Utemini, Manispaa ya Singida, ambapo shughuli za kuuaga mwili wa marehemu zilifanyika, alisema hayuko tayari kutoa taarifa zaidi kutokana na maelekezo kutoka ngazi za juu.

Hata hivyo, taarifa ambazo gazeti hili imezipata kutoka eneo la tukio, zilisema kundi la wananchi wanaokadiriwa kuwa zaidi ya 50 wakiwa na silaha mbalimbali za jadi, walivamia kibanda kimojawapo kilichoko eneo la mgodi, ambacho kinatumiwa na askari polisi na walinzi wa mgodi.

Wananchi hao, kwa mujibu wa taarifa hizo, walianza kushambulia kwa mawe askari wawili waliokuwapo kibandani hapo na ndipo askari mwenzake aliyekuwa na silaha aina ya SMG alitoka na kukimbia mbali na kumwacha mwenzake eneo hilo.

Askari huyo mwenye silaha (jina tunalo) baada ya kuona wananchi waliovamia wanaendelea kushambulia kwenye kibanda hicho, alipiga risasi hewani kuelekea kwenye kibanda kwa nia ya kuwatawanya lakini bahati mbaya baadhi ya risasi zilimpata askari mwenzake, hivyo kupoteza maisha.

Askari huyo aliyefariki dunia ni wa Kikosi cha Kutukiza Ghasia (FFU) cha mjini Singida na ana wiki chache tangu amehamishwa kutoka wilaya ya Mkalama kupelekwa Singida mjini.

Waziri wa Madini, Antony Mavunde, alipofanya ziara katika mgodi huo Oktoba, mwaka jana, aliwataka wamiliki wa migodi nchini kujenga uhusiano mzuri na jamii inayowazunguka na kuwasaidia kuwainua kiuchumi kwa kununua bidhaa wanazozizalisha.

# Mahakama yafuta adhabu kukiri kosa

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, imeifuta kesi ya makubaliano ya kukiri kosa (plea bargain) iliyokuwa imeingiwa kati ya Gasper Swai na Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP) katika kesi ya uhujumu uchumi namba 66 ya mwaka 2018.

Swai alifutiwa kesi hiyo juzi kutokana na maombi madogo ya jinai namba 8 ya mwaka 2023 yaliyofunguliwa katika mahakama hiyo. Kesi hiyo ilikuwa ikisikilizwa na Hakimu Mkazi Mwandamizi Aisha Ndossy.

Hakimu Ndossy alisema ametumia kifungu cha 194 C (1) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20, Marejeo ya Mwaka 2022, kufikia uamuzi huo.

Alisema ameridhika kwamba katika kesi ya uhujumu uchumi namba 66 ya mwaka 2018 iliyokuwa ikimkabili Swai; sheria haikufuatwa wakati wa kuingia makubaliano hayo. Swai alikuwa mtumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) mkoani Arusha.

Swai alikuwa akitetewa na Wakili Peter Madeleka, aliyefungua maombi hayo madogo ya kupinga makubaliano yaliyoingiwa kati yake na DPP.

Kutokana na uamuzi huo, mahakama imefuta 'plea bargain' hiyo pamoja na hatia na adhabu aliyopewa kwenye kesi ya uhujumu uchumi namba 66 ya mwaka 2018.

Hivyo, Swai anatakiwa kurudishiwa fedha zake alizomlipa DPP pamoja na faini aliyolipa mahakamani.

# Msako magari yenye ving'ora, vimulimuli' waja

**Na Christina Mwakangale**

JESHI la Polisi kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani, limepiga marufuku na kutangaza msako wa matumizi ya namba bandia zenye mwinuko '3D' kwenye magari na pikipiki ambazo husababisha kamera zenye mfumo wa madeni kutosoma namba hizo.

Marufuku hiyo inahusu pia wanaofunga ving'ora na vimulimuli huku jeshi hilo likisema ni kinyume cha sheria na kutaka waliofanya hivyo waviondoe kabla ya kukamatwa.

Agizo hilo lilitolewa jana na Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Naibu Kamishna (DCP) Ramadhani Ng'anzi, huku akisema wanatarajia kuanza operesheni kabambe ya kukamata magari yote ambayo si ya dharura lakini yamefungwa ving'ora bila kuzingatia utaratibu wa kisheria.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam alisema: "Kumeibuka tabia ya wenye vyombo vya moto kufunga vifaa ili kushtua watu, madereva wawapishe kwa kudhani ni msafara rasmi.

Pia alisema wapo waliowaka namba za 3D ambazo husababisha kamera zenye mfumo wa madeni kutosoma namba hizo.

"Kuna magari yamefunga ving'ora, vimulimuli na bodaboda ninaagiza makamanda wa vikosi usalama barabarani mikoa yote kukamata kwa magari, bodaboda zilizofunga ving'ora na taa kali bila kufuata utaratibu," alisema Kamanda Ng'anzi

Kamanda Ng'anzi alifafanua mambo mengine yaliyopigwa marufuku ni pamoja na matumizi ya taa zenye rangi na namba zilizo na rangi, akisema zinasababisha kutotambulika kama ni za ndani ya nchi au la.

"Kuna watu wanaweka namba zenye rangi tofauti kinyume cha sheria, bila kujulikana ni za nchi gani. Sisi Jeshi la Polisi namba zetu zilikuwa nyeusi tumeziondoa. Wote wanaofanya hivyo waondoe mara moja," aliongeza.

Aliwataka wamiliki na madereva wote pamoja na wanatoa huduma hiyo nchini kutoweka taa za kuongezwa kwenye magari na pikipiki, tofauti zile ziliwekwa kutoka viwandani.

Alisema hata Shirika la Viwango Tanzania (TBS) limeeleza kwamba, wanaofanya hivyo wanakiuka sheria.

"Kama kuna ulazima wa kufanya hivyo basi anatakiwa kuomba na kupata ridhaa ya kufanya hivyo kutoka kwa Waziri wa Mambo ya Ndani mwenye dhamana ya kuidhinisha vibali hivyo. Ving'ora hufungwa katika pikipiki iwapo imetengenezwa kwa kusudi maalumu.

"Sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168 kama ilivyopitiwa mwaka 2002 kifungu cha 54 (2) (5), king'ora kitafungwa kwenye gari au pikipiki za dharula (Emergency Motor Vehicle) tu katika misafara ya viongozi, pikipiki za polisi, zimamoto, hospitali na pikipiki za jeshi, kwa kuzingatia maelekezo ya waziri," alisema.

Kamanda Ng'anzi alisema wapo watu binafsi, kampuni au taasisi zinazofunga ving'ora katika magari yao na kuvitumia bila kuzingatia utaratibu.

Alisema kufanya hivyo ni uvunjifu wa sheria na wanastahili adhabu ikiwamo ya kulipa faini ya tozo za makosa va usalama barabarani au kuwekwa mahabusu na kuandaliwa mashtaka na kupelekwa mahakamani au vyote kwa pamoja.

"Kuna baadhi ya watu wanafunga taa zenye mwanga mkali zinazoongezwa kwenye magari au pikipiki yaani 'Spot light' na 'Led bar' kama urembo kwenye magari na pikipiki, kwa kufanya hivyo wanatakiwa wavitoe mara moja.

"Baadhi watu wamejenga utamaduni na wamejihalalishia kuwa ni sheria kuweka namba za bandia katika magari. Kufanya hivyo ni kinyume na sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168 kama ilivyopitiwa mwaka 2002 kifungu cha 8. Azitoe mwenyewe kwa hiari yake." Aliagiza.

Alisema iwapo magari hayo yamewekwa taa hizo kutoka kiwandani maana yake zinaruhusiwa na matumizi yake yawe ni sehemu za migodi na kwenye mapori pekee wakati wa uwindaji na si vinginevyo, ili kuepusha ajali za barabarani kutokana na matumizi ya taa zenye mwanga mkali.

HABARI KITAIFA

# Kilichombeba mjane wa Bilionea Msuya kuachiwa

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam, imemwachia huru mjane wa aliyekuwa mfanyabiashara wa madini mkoani Arusha, Erasto Msuya, maarufu kama Bilionea Msuya, Miriam Mrita, na mwenzake Revocatus Everist Muyella maarufu kama Ray.

Mrita na Muyella walikuwa wanakabaliwa na kesi ya mauaji ya dada wa Bilionea Msuya, Anneth, aliyeuawa Mei 26, 2016 kwa kuchinjwa nyumbani kwake Kibada, Kigamboni mkoani Dar es Salaam.

Washtakiwa hao waliachiwa huru baada ya kusota mahabusu kwa zaidi ya miaka saba kutokana na upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha mashtaka dhidi yao. Mrita alipandishwa kizimbani kwa mara ya kwanza katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam Agosti 23,2016.

Hukumu hiyo iliyosomwa kuanzia saa 5:01 asubuhi hadi saa 1:07 jioni na Jaji Edwin Kakolaki, ilisababisha vilio vya furaha na vya simazi kwa ndugu, jamaa na marafiki waliofika katika chumba cha wazi namba moja cha mahakama hiyo, ambacho kilikuwa kimetawala ukimya muda wote hadi pale washtakiwa walipoachiwa huru.

“Mahakama imejiridhisha kwamba upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha mashtaka dhidi ya washitakiwa. Mahakama inawaona hawana hatia, hivyo inawaachia huru kwa kosa linalowakabili na ninaelekeza huko gerezani wawaachie labda kama wana makosa mengine,” alisema Jaji Kakolaki

Baada ya Jaji Kakolaki kusema kwamba mahakama imeridhika kwamba upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha mashtaka bila kuacha shaka yoyote, ukimya ulipotea na maneno “Yesu umetenda” na “damu ya mtu iliyomwagika italipwa” yakasikika.

Furaha hizo na majonzi zilimfanya Jaji Kakolaki asiendelee kumaliza kutoa hukumu yake kutokana na kuwapo kwa kelele ndani ya chumba cha mahakama, mjane akiwa ndani ya kizimba alilala chini huku akilia kwa uchungu akimshukuru Mungu kwa kuachiwa huru. Askari Magereza alimwinua ili kuweka utulivu Jaji aendelee.

Ghafla, dada wa marehemu Aneth, ambaye hakufahamika jina alipiga kelele akiwa kwenye benchi la mahakama na kisha akaanguka chini akilia kwa uchungu kwa kusema damu ya Aneth watailipa wote waliohusika kisha akaanza kugalagala chini huku Jaji akiwa bado hajatoka nje ya chumba cha mahakama na bado alikuwa hajamaliza kusoma hukumu.



Mjane wa aliyekuwa mfanyabiashara wa madini, Erasto Msuya maarufu Bilionea Msuya, Miriam Mrita na mwenzake Revocatus Muyella maarufu Ray, wakiwa kizimbani kabla ya kuachiliwa huru na Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

Askari wa kike alimfuata dada huyo na kumwambia mahakama inaendelea, hivyo anatakiwa aache kelele na aende nje, akaanza kuzungumza kwa sauti kubwa huku akilia kwa uchungu kwamba haogopi kufungwa kwa sababu ndugu zake wameshauawa.

Wakati kiendelea kupiga kelele akidai kuwa wamfunge tu haogopi kitu chochote, ndugu wa Mrita ambao walikaa upande wa kulia wa chumba hicho, walinyamaza kimya kusikiliza kinachofuata huku ndugu wa marehemu Aneth waliokuwa wamekaa upande wa kushoto, walikuwa wamejitenga.

Baada ya ukimya, Jaji Kakolaki alimalizia hukumu kwa kusema kuwa gari aina ya Range Rover ambalo lilitolewa mahakamani kama kielelezo litaifishwe kuwa mali ya serikali kwa sababu halina mtu hata katika mirathi gari hilo halimo.

Jaji huyo tangu aingie mahakamani hakuinuka kutoka katika kiti chake, licha ya washtakiwa na watu wengine kutoka nje ya chumba hicho kwa ajili ya kujinyoosha mwili na kwenda msalani. Hata ilipofika saa 11:34 jioni, jua lilifika kwenye kiti chake, akatumia mkono wake kujiziba juu kidogo ya miwani yake ili kuendelea kuchambua ushahidi wa kesi hiyo.

Tukio hilo lilidumu ndani ya dakika tatu kuanzia saa 11:35 hadi saa 11:37 jioni na hali hiyo ilimwathiri kuendelea kuchambua ushahidi wakati huo chumba cha mahakama kikiwa kimya kama hakina watu kutokana na kila mmoja sikio lake kuwapo kwa Jaji.

Hakukuwa na minong'ono wala kelele zozote, ni sauti tu za mbavu za watu wakijinyoosha katika mabenchi ya mahakama kutokana na uchovu huku wakinywa maji taratibu wakisubiri hukumu imalizike kusomwa.

**SABABU KUACHIWA**

Wakati Jaji Kakolaki akitoa sababu za kuwaachia huru, alisema upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha kama mjane huyo alikuwapo eneo la tukio na kwamba hakuna muunganiko wowote wa ushahidi unaomtia hatiani.

“Ili Mrita aweze kuunganishwa katika mauaji hayo, upande wa mashtaka ulitakiwa kuchukua sampuli ya vielelezo vilivyokuwapo katika tukio ili viweze kuunganishwa na sampuli za mshtakiwa kwa sababu vinasaba vinaeleza kwamba damu iliyokuwamo kwenye kisu ni ya jinsia ya kike, lakini haikusemwa ni ya nani,”alisema.

Pia alisema mahakama imebaki na shaka kama kisu kilichotumika kumchinja Aneth ndicho kilichokutwa eneo la tukio kutokana na kwamba vinasaba vinaonyesha mshtakiwa wa pili, Muyela, vinafanana na vinasaba vya kwenye kisu na filimbi, kwa hiyo inawezekana yeye ndiye aliyefikisha eneo la tukio au kuvitumia.

Hata hivyo, mahakama ilitupilia mbali hoja 10 za upande wa utetezi za mawakili Peter Kibatala na Nehemiah Nkoko kwamba ushahidi wa shahidi namba 25 Getruda Mfuru dada wa kazi wa marehemu Aneth kwamba ulikuwa na shaka.

Pia jaji huyo alitupilia mbali hoja za upande wa utetezi kuhusiana na tarehe ya Aneth kufariki dunia kwa sababu mahakama imejiridhisha kupitia daktari aliyeufanyia uchunguzi mwili alisema kifo kilitokea ndani ya masaa 24 na pia kuhusu hati ya mashtaka hakuwa na tatizo lolote.

Hukumu hii imesomwa na Jaji Kakolaki wa mahakama hiyo, baada kumaliza kupitia ushahidi wa mashahidi 25 wa upande wa mashtaka, mashahidi watano wa utetezi, vielelezo 31 na kupitia vifungu vya sheria.

Upande wa mashtaka katika kesi hiyo uliongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Paul Kimweri, akisaidiana na Yasinta Peter , Marietha Maguta na Generosa Montano.

Baada ya askari Magereza kuwaachia washtakiwa, ndugu, jamaa na marafiki walitoka katika eneo la mahakama kwa nyimbo za mapambio huku wakimsindikiza Mrita katika gari aina ya Range Rover kisha kuondoka huku wakipanda magari tofauti na mshtakiwa wa pili Muyela.

Akizungumza na waandishi wa habari, Wakili Kibatala alisema anamshukuru Mungu mteja wake Mrita ametoka akiwa na afya lakini Muyela kwa bahati mbaya amepata tatizo la kiafya.

“Naishukuru Mahakama kwa kukubaliana na hoja zetu. Kama mnavyoona imewaachia huru washtakiwa wote. Ndugu zangu wa Arusha nawaletea dada yenu, wifi yenu, shemeji yenu. Sina tena deni kwenu,”alisema

**MAJUMUISHO WAZEE**

Desemba 11,2023 wakati wazee wa baraza (Iddi Humba na Omary Panzi) wanatoa maoni yao, waliishauri mahakama iwaachie huru washtakiwa kwa madai kuwa hawana hatia.

Mzee Humba alidai kuwa amepitia ushahidi wa mashahidi 25 na ushahidi wa upande wa utetezi wa mashahidi watano wa utetezi na kujiridhisha kwamba upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha shtaka bila kuacha shaka yoyote.

Jaji Kakolaki baada ya kusoma muhtasari wa ushahidi wa kila shahidi wa pande zote, alisema katika jinai, kuna mambo makuu mawili ya kuangalia kitendo chenyewe ambacho mshtakiwa anakuwa anatuhumiwa kukitenda na kwamba lazima kiwepo kitendo hicho kithibitike.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
28.02.2024

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **01.03.2024 hadi 07.03.2024** kampuni ya **CEVA Interfreight** itasafirisha mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Bandari ya Dar Es Salaam** kuelekea **Mzenga,** gari hilo lenye namba za usajili **NRB97300 / NRB15200 DS00TG GP / NRB43293**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **Mita** | **36.50** |
| **Upana** | - | **Mita** | **7.40** |
| **Kimo** | - | **Mita** | **4.70** |

3. Njia itakayotumika: **Bandari ya Dar Es Salaam hadi Mzenga** kupitia **Barabara ya Mandela, Barabara ya Morogoro mpaka Mlandizi,** magari yatasafiri muda wa usiku ***( Kuanzia saa 08:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri).*** Kutoka Mlandizi kwenda Mzenga magari yatasafiri muda wa mchana ***( Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni).***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

117850202



Mabaki ya gari aina ya Toyota Land cruiser lenye namba za usajili STL 9035 baada ya kupata ajali likiwa katika msafara wa Naibu Waziri Mkuu, Doto Biteko wilayani Mufindi, mkoani Iringa juzi.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Msafara wa Biteko wapata ajali

**Na Mwandishi Wetu,** IRINGA

GARI aina ya Toyota lenye namba za usajili STL 9035 lililokuwa katika msafara wa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, limepata ajali na mtu mmoja amefariki dunia na wengine wawili kujeruhiwa.

Ajali hiyo ilitokea juzi saa moja usiku katika eneo la Mlolo, wilayani Iringa, barabara kuu Iringa-Mbeya wakati msafara wa Dk. Biteko ukitoka kijiji cha Mkangwe, wilayani Mufindi kuwasha umeme.

Januari 26, mwaka huu, watu wawili ambao ni mwandishi wa habari Kituo cha Televisheni Tanga, (TaTV), Ally Haroun na dereva wa gari la Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Tanga (Tanga UWASA), Said Alawi, walifariki dunia na wengine wanne kujeruhiwa katika msafara wa Dk. Biteko katika kijiji cha Mamboleo barabara ya Tanga-Segera.

Juzi, Nipashe ilifika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Iringa na kushuhudia magari saba yaliyokuwapo katika msafara wa Dk. Biteko yakiwa eneo la wagonjwa wan je (OPD).

Mmoja wa madereva wa magari hayo, akizungumza kwa sharti la kutoandikwa jina gazetini, alisema gari lililopata ajali lilikuwa na maofisa watatu na alishuhudia ilivyotokea.

Alisema abiria aliyekuwa amekaa kiti cha mbele ndiye aliyefariki dunia huku dereva na ofisa mwingine wakijeruhiwa.

Nipashe ilipomtafuta kwa njia ya simu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Iringa, Dk. Alfred Mwakalebela, iliita bila kupokewa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Allan Bukumbi, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo na kusema wanaendelea kufuatilia.

"Ni kweli ajali imetokea. Kuna gari lilifuatana na msafara huo limepata ajali ila halijulikani ni la idara gani RTO (Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani wa Mkoa) amekwenda kufuatilia nitakupatia taarifa kamili usiku huu," alisema Kamanda Bukumbi. Msafara wa Dk. Biteko ulikuwa ukitokea kuwasha umeme Kijiji Cha Mkangwe, Kata ya Idunda na kufanya vijiji vyote 360 ndani ya Mkoa wa Iringa kupata umeme.

# Udumavu bado ni pasua kichwa

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

SERIKALI mkoani Rukwa imesema tatizo la udumavu bado ni kubwa, hivyo kuwaomba wadau, wakiwamo wanahabari kushiriki katika mikakati ya kuutokomeza.

Kwa mujibu wa takwimu, tatizo hilo kwa sasa limefikia asilimia 50, hivyo kusababisha athari kubwa kwa Watoto.

Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa (Uchumi na Uwezeshaji), Salehe Msanda, alibainisha hayo jana wakati akizungumza na wanahabari aliokutana nao kwa lengo la kuweka mikakati ya pamoja katika kukabiliana na tatizo hilo.

Alisema katika mkoa hali ya udumavu imefikia asilimia 50 wakati kiwango cha kitaifa ni asilimia 30.4 huku ukondefu ukiwa ni asilimia 19.4 wakati kitaifa ni asilimia 12.

Msanda alisema kuwa takwimu pia zinaonyesha kuwa tatizo la uzito uliopitiliza limefikia asilimia 3.2 wakati kitaifa ni asilimia 3.5 na tatizo la uzito mdogo limefikia asilimia 8.3 huku kitaifa ikiwa asilimia 3.2.

Alisema Rukwa ni kati ya mikoa saba inayoongoza kwa kuzalisha mazao ya nafaka pamoja na mazao mengine ya chakula na katika msimu wa kilimo uliopita, ulikuwa wa pili katika uzalishaji wa chakula nchini lakini bado unakabiliwa na udumavu mkubwa.

"Mahudhurio ya wajawazito kliniki ni zaidi ya asilimia 90 pia watoto wamekuwa wakipata chanjo kwa zaidi ya asilimia 90 lakini kumekuwa na changamoto ya udumavu pamoja na hizo nyinginezo, hivyo mkoa umeandaa mikakati mbalimbali ya kukabiliana na suala hilo," alisema. Awali, Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Makongoro Nyerere, alisema tatizo la udumavu limekuwa likiathiri zaidi sekta ya elimu na matokeo ya wanafunzi yamekuwa mabaya katika mitihani ya kitaifa.

Alisema katika matokeo ya darasa la saba yaliyopita, zaidi ya wanafunzi 600 walifeli na hii inachangiwa na sababu mbalimbali ikiwamo udumavu ambao unasababisha ubongo wa watoto kutokukua na kufanya kazi vizuri.

Mkuu huyo wa mkoa alisema ni lazima wataalamu wa lishe watoe elimu kwa wazazi ili katika siku 1,000 tangu kuzaliwa kwa mtoto wapate chakula bora chenye viinilishe kamili ili viwasaidie kukua vizuri kwa ubongo.

Kutooan ana tatizo hilo, alisema mkoa utazindua kampeni maalumu kwa ajili ya kutoa elimu ya lishe kwa kuwa kaatika mkoa vyakula vipo vingi lakini tatizo ni baadhi ya wananchi kutojua namna ya kuandaa na kula vyakula hivyo.

# AfDB yaipatia Tanzania mkopo wa bil. 399/- ujenzi SGR, mtaji TADB

**Na Gwamaka Alipipi**

BENKI ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imeipatia Tanzania mkopo wa Dola za Marekani milioni 158.1 (Sh.bilioni 398.7) kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Tabora hadi Burundi pamoja na uwezeshaji mtaji Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB).

Akizungumza wakati wa hafla ya kutia saini mikataba hiyo jijini Dar es Salaam jana, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema malengo ya miradi hiyo ni mwendelezo wa utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025 na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021-2026.

Alisema kati ya fedha hizo, Dola za Marekani milioni 91.76 (Sh. bilioni 231.3) ni mkopo wa ujenzi wa reli ya kisasa kipande cha sita (kilometa 411) kutoka Tabora hadi Kigoma na kipande cha saba (kilometa 156) kutoka Uvinza hadi Malagarasi. Dk. Nchemba alisema mradi huo utatekelezwa kwa kipindi cha miaka saba kuanzia mwaka 2024 hadi 2031.

"Uwekezaji huu wa reli, utawezesha kuunganishwa na Bandari ya Dar es Salaam kupitia mradi unaondelea wa ujenzi wa Reli SGR kutoka Dar es Salaam - Morogoro - Makutupora - Isaka - Tabora, lengo likiwa ni kuiunganisha Tanzania na nchi ya Burundi," alisema. Kadhalika, Mwigulu alisema Dola za Marekani milioni 66 (Sh. bilioni 166.4) zilaelekezwa TADB kwa ajili ya kusaidia kukuza mtaji.

Alisema fedha hizo zinalenga kuwezesha Watanzania kupata mitaji kwa ajili ya shughuli za kilimo inayolenga kuongeza uzalishaji, kuimarisha usalama wa chakula.

Pia alisema itawezesha kukuza biashara ya bidhaa zinazouzwa ndani na nje ya nchi pamoja na kuongeza ajira zitakazoinua uchumi katika ngazi ya mtu mmoja, familia na taifa.

"Kupitia ongezeko hili la mtaji, tunategemea TADB itaongeza fursa ya upatikanaji wa mikopo kwa makundi ya vijana kupitia Mpango wa BBT unaoendelea kutekelezwa na Serikali kupitia Wizara ya Kilimo," alisema.

Meneja Mkazi wa AfDB Tanzania, Dk. Patricia Laverley, alisema lengo la mkopo huo ni kuimarisha sekta ya usafiri na usafirishaji kwa Watanzania.

Alisema ni matumaini kwa AfDB baada ya kutoa fedha hizo na mradi ya ujenzi wa Reli ya Kisasa kumalizika utakwenda kuondoa msongamano wa malori yanayobeba mizigo kuelekea mkoani Kigoma na nchi jirani.

Kuhusu mkopo wa sekta ya kilimo, Dk. Laverley alisema ni matumaini ya AfDB kwamba unakwenda kuleta mabadiliko chanya katika sekta ya kilimo.

Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alisema kukamilika kwa ujenzi wa Reli ya Uvinza hadi Musongati kutawezesha kufikia mgodi mkubwa wa madini ya nickel uliopo Musongati nchini Burundi.

Alisema mgodi huo una hifadhi ya tani milioni 150 za madini ya nickel, cobalt na shaba kwamba reli hiyo inatarajiwa kusafirisha madini tani milioni tatu kwa mwaka.

# TIC, CRDB kushirikiana kukuza uwekezaji

**Na Joseph Mwendapoe**

KITUO cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kimeweka lengo la kuongeza idadi ya miradi ya uwekezaji kwa Watanzania kufikia miradi 1,000 kufikia mwishoni mwa mwaka huu.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Gilead Teri, wakati wa kutia saini makubaliano ya ushirikiano na benki ya CRDB kuhusu kukuza uwekezaji nchini.

"Nina furaha kubwa kusimama hapa mbele yenu kushukuru benki ya CRDB kuona umuhimu wa kukuza na kuboresha uendeshaji wa masuala ya kiuwekezaji nchi, sisi sote ni mashahidi katika hili na hivi karibuni tumeshuhudia mabadiliko makubwa katika uwekezaji," alisema.

Teri alisema mwamko wa uwekezaji nchini umekuwa kwa kasi na kuleta tija katika uchumi wa Watanzania na taifa kwa ujumla na kwamba mwaka 2023, TIC ilisajili miradi ya 504 yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 4.6 bilioni na kutoa ajira zinazokadiriwa kuwa zaidi ya 230,000.

Alisema kupitia kampeni ya uwekezaji inayoendelea, TIC imejiwekea malengo ya kuongeza idadi ya miradi ya uwekezaji maradufu na kufikia miradi ya Watanzania 1000 ifikapo mwishoni mwa mwaka 2024.

Kwa mujibu wa Teri, wamekubaliana na CRDB kushirikiana katika teknolojia na ubunifu ili kuvutia na kuhudumia wawekezaji kwa njia bora zaidi.

"Kwanza kabisa, tunaangazia ubunifu katika kutoa huduma mbalimbali kwa wawekezaji. Tunatambua kuwa mahitaji ya wawekezaji yanabadilika na kuhitaji huduma za kibunifu na zenye ubora wa hali ya juu na kupitia ushirikiano wetu na CRDB. Tunalenga kutoa huduma mbalimbali za kifedha na kiufundi zenye ubunifu ili kuhakikisha kuwa wawekezaji wanapata suluhisho bora zaidi kulingana na mahitaji yao," alisema Teri.

Pia alisema wanatarajia kuboresha mifumo yao ya usajili wa miradi ya wawekezaji na wanaamini kuwa njia za usajili zilizorahisishwa kiteknolojia zitavutia wawekezaji wengi zaidi.

Alisema kupitia ushirikiano na Benki ya CRDB, wataimarisha mifumo ya malipo kwa kuongeza njia za kidigitali (e-commerce and POS).

"Tunatambua umuhimu wa mifumo ya malipo salama, haraka na inayoweza kupatikana kwa urahisi kwa wawekezaji. Kwa ushirikiano huu wawekezaji wataweza kupata huduma mbalimbali za kibenki bora na salama," alisema

TIC, alisema inatambua kuwa uhusiano mzuri na wateja ni muhimu katika kuvutia na kudumisha uaminifu wa wawekezaji na kwamba kupitia ushirikiano huo na CRDB, wanalenga kuanzisha mifumo ya kisasa ya usimamizi wa uhusiano na wateja ili kuhakikisha kuwa mahitaji yao yanatimizwa kikamilifu na wanapata msaada unaostahili.

"Tunaelekeza juhudi zetu katika kuongeza ubunifu katika uhamasishaji wawekezaji wa ndani na tunatambua umuhimu wa kuhamasisha wawekezaji wa ndani na kujenga uwezo wao wa kushiriki katika miradi ya uwekezaji," alisema.

Aidha, alisema kupitia ushirikiano huo, TIC inalenga kuanzisha programu za ubunifu za uhamasishaji na mafunzo kwa wawekezaji wa ndani ili kuwawezesha kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya uchumi wa nchi.




Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo (katikati), akipokea mashuka 500 kutoka kwa Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Dar es Salaam, Dismas Prosper (wapili kushoto) yaliyotolewa na Benki ya hiyo kwa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi hiyo, Dk. Peter Kisenge, Mwenyekiti wa Chama cha Wanawake cha Taasisi hiyo, Dk. Angella Mutuzya (kulia) na Meneja wa Benki hiyo, Tawi la Muhimbili, Frank Makungu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benki yaipiga jeki JKCI vifaa vya mil.9/-

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imekabidhi mashuka 500 yenye thamani ya Sh. milioni 9 kwa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) ili kuboresha mazingira kwa wagonjwa.

Akizungumza jana katika hafla fupi ya makabidhiano iliyofanyika katika taasisi hiyo jijini Dar es Salaam, Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Dismas Prosper, alisema msaada huo ni utekelezaji wa mkakati wa benki hiyo katika uwajibikaji kwa jamii (CSR).

"Kwa zaidi ya miaka saba sasa, benki yetu iliridhia kurudisha asilimia moja ya faida yetu kila mwaka katika kuchangia maendeleo ya jamii inayotuzunguka na sekta ya afya ni miongoni mwa vipaumbele vyetu vikuu. Tuna furaha kuwa leo (jana) tunakabidhi mashuka 500 kwa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete na tunaamini kuwa msaada huu utasaida kuboresha mazingira kwa wagonjwa," alisema.

Prosper aliahidi kuwa benki inatendelea kufanya kazi na serikali kwa karibu kwa kutambua kuwa sekta ya afya ni nyenzo muhimu katika kuchochea maendeleo ya nchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge, aliushukuru uongozi wa NMB kwa msaada huo huku akibainisha kuwa taasisi yake imendelea kuimarika zaidi kutokana na michango mingi inayotolewa na wadau.

"Miongoni mwa wadau hao ni NMB. Benki hii imekuwa ikitoa kipaumbele katika maendeleo ya taasisi yetu kwa kutoa michango mbalimbali. Nia ya serikali yetu ni kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma bora bila kujali ana uwezo gani," alisema.

Alisema taasisi yake miaka michache ilaanzisha mpango maalum wa 'Mama Samia Outreach Program' ambao tayari umeweza kuwafikia watu 12,000 katika mikoa 12 nchini.

Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, aliishukuru NMB kwa kuendelea kuchangia jitihada mbalimbli za maendeleo za serikali huku akizitaka kampuni na taaisi nyingine kuiga mfano huo.

"Ziko taasisi nyingi zinazopata faida katika mkoa wetu wa Dar es Salaam na zote zingekuwa zinawajibika ipasavyo kama NMB, basi mkoa wetu ungepiga hatua kubwa zaidi kimaendeleo," alisisitiza.

Awali, Mkurugenzi wa Upasuaji wa JKCI, Angela Muhozya, ambae pia ni Kiongozi wa Umoja wa Wanawake JKCI alibainisha kuwa msaada huo ni utekelezaji wa ombi la umoja wao kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, mwaka jana.

## Waonya hatari ya kulala na jiko mkaa

**Na Mary Geofrey**

MKAA ambao haujaungua ukaisha vizuri, umetajwa kuwa chanzo cha kuzalisha sumu aina ya Carbonmonoxide inayosababisha kifo kwa atayelala na jiko lenye moto wa mkaa ndani.

Msimamizi wa Kituo cha Taifa cha Kudhibiti Matukio ya Sumu wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), Yohana Goshashy, alibainisha hayo jana mkoani Iringa kupitia taarifa iliyotumwa kwa vyombo vya habari.

Goshashy alikuwa akizungumza na wenyeviti wa mitaa, maofisa afya na mazingira na wahudumu wa afya ngazi ya jamii kuhusu namna ya kudhibiti matukio ya sumu kwenye jamii.

Goshashy alisema wananchi wengi hawafahamu kuhusu madhara ya moto huo na wamekuwa wakiendelea kuishi nao ndani ya nyumba zao hali inayoweza kusababisha kifo.

Aidha, alihimiza jamii kujenga nyumba zenye sehemu mbalimbali za kupitisha hela ili kuondokana na hatari hiyo.

"Tupo Iringa kwa ajili ya kutoa elimu kwa jamii kupitia viongozi hawa wa ngazi ya jamii, namna ya kuepuka vifo vinazotokana na sumu aina ya Carbon Monoxide inayotengenezwa na moto wa mkaa usioungua na kuisha. Hivyo," alisema.

Mganga Mkuu wa Manispaa ya Iringa, Dk. Godfrey Mbangali, aliwataka viongozi wa serikali za mitaa, watoa elimu ya afya kwa jamii na maofisa afya mazingira ngazi ya kata kutoa elimu kwa jamii kuhusu matukio ya sumu ili kulinda afya ya jamii na kupunguza vifo vitokanavyo na madhara ya sumu.

"Niwasihi washiriki wa mafunzo haya mkawe mabalozi katika kupunguza na kudhibiti matukio ya sumu katika maeneo yenu ya kazi jamii inayowazunguka na sehemu zingine yatakapotokea matukio ya sumu.

"Tuhakikishe tunakuwa tayari muda wote, kwani matukio ya sumu ni matukio ya dharura, hivyo utayari wenu wa utoaji huduma au taarifa kwa aliyepatwa na tukio la sumu utasaidia upatikanaji wa huduma stahiki aliyedhurika," alisema Dk. Mbangali.

Aidha, Mganga Mkuu aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kuwa katika nafasi nzuri ya kusambaza elimu kuhusu masuala mbalimbali ya sumu kwa jamii inayowazunguka na pia, kushirikiana na Kituo cha Taifa cha Kudhibiti Matukio ya Sumu ya Carbon Monoxide.

Muhudumu wa Afya Kata ya kwa Kilosa, Khadija Mili, aliishukuru mamlaka kwa kutoa elimu ya sumu Manispaa ya Iringa na kusema kuwa, masuala ya sumu yanaepukika hivyo, wapo tayari kueneza elimu ya kudhibiti matukio ya sumu kwa jamii wanayoihudumia.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga bado kazi haijaisha CAF

**WIKI** hii tunashuhudia michezo ya Kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika inayoendelea katika nchi tofauti tofauti Afrika, Tanzania ikiwa moja ya nchi inayoshuhudia michezo hiyo.

Kwa hapa nyumbani Tanzania, timu zetu kongwe, Simba na Yanga nazo zipo kwenye michuano hii hatua ya makundi zikipambana kusaka nafasi ya kutinga hatua ya robo fainali ya michuano hii mikubwa Afrika.

Simba jana usiku ilikuwa ugenini kucheza mchezo wake wa marudiano dhidi ya wenyeji wao Asec Mimosas ya nchini humo, ikumbukwe mchezo wa kwanza wa timu hizo uliochezwa mwaka jana kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa timu hizo zilifungana bao 1-1.

Lakini pia leo wawakilishi wetu wengine kwenye michuano hiyo, Yanga nao wanaingia uwanjani kucheza na CR Belouizdad mchezo muhimu wa kusaka nafasi ya kutinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.

Mchezo wa kwanza wakiwa ugenini Yanga walikubali kipigo cha mabao 3-0 hivyo leo mbali na kusaka ushindi utakaowaweka katika nafasi nzuri kwenye kundi lao, lakini pia watataka kulipiza kisasi kwa waarabu hao.

Kimsingi timu zetu hizi zinapaswa kujua kazi bado haijaisha bila kujali matokeo gani watayapata ingawa matokeo ya ushindi yatawaweka kwenye nafasi nzuri zaidi ya kutinga hatua ya robo fainali.

Wachezaji na benchi la ufundi hawapaswi kukata tama wala kubweteka kwa matokeo yao, wanapaswa kujua bado kuna michezo miwili mbele yao ambayo inaweza ikaamua hatma yao msimu huu.

Kitu kikubwa na cha kipekee ni kuhakikisha wanamaliza vizuri mechi zao zilizobakia hili Tanzania iweke rekodi ya kuingiza timu mbili kwenye hatua ya robo fainali ya michuano hiyo mikubwa zaidi kwa ngazi ya vilabu Afrika.

Tunawakumbusha wachezaji wa vilabu hivi viwili kuwa kazi bado haijaisha, bado wana kazi ya kufanya katika michezo miwili iliyobakia hili kujua hatma yao kuelekea robo fainali ya klabu bingwa Afrika.

Baada ya mchezo wa jana, Simba wamebakisha michezo miwili, mmoja watacheza nyumbani na mmoja ugenini. Wataanza kwa kucheza na Jwaneng Galaxy ya Botswana kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es salaam.

Baada ya mchezo huo watasafiri kwenda Morocco kucheza na Wydad Casablanca mchezo wa mwisho hatua ya makundi, umuhimu wa mchezo huu utatokana na matokeo watakayoyapata kwenye mchezo dhidi ya Jwaneng, ndio maana tunasema kazi bado haijaisha.

Hivyo hivyo kwa upande wa Yanga, baada ya mchezo wa leo itakuwa imebakisha michezo miwili katika hatua hiyo ya makundi, itakuwa na mchezo dhidi ya Medeama ya Ghana mchezo utakaochezwa uwanja wa Benjamin Mkapa.


Baada ya mchezo huo Yanga watasafiri kwenda Misri kucheza na Al Ahly, pia kama ilivyo kwa Simba, umuhimu wa mchezo huu utatokana na matokeo watakayoyapata kwenye mchezo wa leo na ule wa Medeama, kazi bado haijaisha.

Kikubwa lazima benchi la ufundi na wachezaji wajidhatiti kuhakikisha wanafanya vizuri kwenye mechi hizo zilizobakia na wajue hatma yao ya kusonga mbele pia itatokana na matokeo watakayoyapata.

Hatuwezi kuficha, msimu huu wa mashindano ya CAF kwa ngazi ya vilabu Tanzania imeweka rekodi kwa nchi za ukanda wa CECAFA kwa kushuhudia klabu zake mbili zikitinga hatua ya makundi.

Itakuwa rekodi nyingine kama timu zote za Simba na Yanga zitatinga hatua ya rekodi na hivyo kuendelea kuipaisha nchi pamoja na ligi yetu ya NBC.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Muungwana Lazima Nilonge

Na Adam Fungamwango

# Simba na Yanga haziwezi kuungana, ila zisihujumiane

**KWA** jinsi ninavyoufahamu mpira wa Tanzania, mashabiki wa soka wa nchi hii na tabia zao, pamoja na siasa zake, hakuna hata siku moja ambayo wanachama, mashabiki na hata viongozi wa klabu za Simba na Yanga wataungana ili kuisaidia timu moja wapo kupata ushindi, au kuishangilia timu moja wapo zitakapokuwa zinacheza mechi za kimataifa.

Hata kama viongozi na wanasiasa watatumia ushawishi wao kuwakusanya na kukaa pamoja eti upande mmoja umshangilie mwingine, utafanya hivyo kinafiki na si kutoka ndani ya mioyo yao.

Binafsi nimepata kushuhudia mwaka 1993 wakati Simba ilipocheza fainali ya Kombe la Shirikisho na Mpira wa Miguu Afrika (CAF), dhidi ya Stella Abidjan ya Ivory Coast, Uwanja wa Taifa jijini Dar es salaam (sasa Uhuru), kutokana na umuhimu wa mechi hiyo, wanasiasa wote na viongozi waliungana na kuanza kuwashawishi wanachama na mashabiki wa Yanga kuwaunga mkono wenzao Simba kuishangilia.

Katika mechi ile kama Simba ingeshinda ingeiweka Tanzania kwenye rekodi nzuri kwenye soka la Afrika.

Walifanikiwa kuwakusanya, lakini kwangu mimi nasema ni kinafiki. Ndiyo, nasema hivyo kwa sababu wakati Jean Bolizozo alipofunga bao la pili na kusitisha ndoto za Simba kutwaa ubingwa ikichapwa mabao 2-0 nyumbani, wanachama na mashabiki wa Yanga walionyesha rangi yao halisi walipogeuka na kuanza kuimba, "uzalendo umetushinda, uzalendo umetushinda."

Ndiyo, hawakuwa na kosa! Walilazimishwa, hawakuwa na mapenzi na Simba moyoni mwao. Mapenzi hayalazimishwi.

Nimeona hata majuzi baadhi ya viongozi wakiwasihi wanachama na mashabiki wa timu hizo kuungana hasa timu zao zinapocheza mechi za kimataifa.

Huu umekuwa wimbo unaojirudiarudia, huwa tunausikia mara nyingi timu za Simba na Yanga zinapocheza mechi za kimataifa, hata hivyo hakuna kinachoendelea wala kufanyika.

Ndiyo kwanza tunaona baadhi ya timu zikienda kupokea hata wageni Uwanja wa Ndege wa Kimataifa.

Binafsi mimi naona ifike mwisho tuwaache mashabiki nini wanataka kuliko kuwalazimisha kuungana.

Shabiki wa Yanga akienda kushangilia timu ngeni uwanjani aachwe, kwa sababu amekwenda mwenyewe, ameingia kwa pesa yake, ana haki ya kushangilia timu yoyote.

Wa Simba naye hivyo hivyo, ana haki ya kushangilia timu yoyote anayoipenda kwani hajapelekwa na mtu.

Tuachane na tabia za kinafiki, kila mmoja aachwe ashangilie anachotaka kwa sababu ni ngumu sana kuwaunganisha mashabiki wa timu hizi mbili.

Wote wana tabia kama za baadhi ya kinadada wa uswahilini. Hawataki kuona mwenzao akila vizuri, akinawiri, akivaa vizuri, watanuna tu, wanamnunia, wanamteta na kumuundia zengwe.

Kila mmoja anataka yeye ndiye apate mwenzake akose. Hii ndiyo furaha hata za watu wa Simba na Yanga.

Kitu ambacho nadhani ni kibaya, ambacho Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Serikali kupitia Mamlaka zake za Jeshi la Polisi, TCRA, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Usalama wa Taifa, kuhakikisha timu yoyote kati ya hizo haihujumiwi na mwenzake au yoyote yule inapojiandaa au kwenda kucheza mechi za kimataifa.

Kumekuwa na minong'ono kuwa imefika hatua mpaka timu hizi zimekuwa na tabia ya kuhujumiana ili mmoja asifanye vizuri kwa sababu tu wasichekane.

Kwangu mimi hata kuwapokea wageni Uwanja wa Ndege ni kitendo ya hujuma, hakipaswi kufumbiwa macho.

Nadhani viongozi wetu na wasasiasa wangejielekeza huko, kuziambia mamlaka hizo kuzilinda timu kwenye hujuma tunasozisikia na kuambiwa, inapaswa kupambana na wote wanaobainika kufanya hivyo, lakini siyo kuwalazimisha mashabiki kushangilia timu ambazo hazipo mioyoni mwao.

HABARI KITAIFA

# EPZA kufanya tathmini ya viwanda

Na Mwandishi Wetu

MAMLAKA ya Mauzo ya Bidhaa Nje ya Nchi (EPZA), imeamua kufanya tathmini ya viwanda vyake nchi nzima kwa lengo la kuboresha kanzidata yake.

Mkuu wa Kitengo Cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma wa EPZA. Panduka Yonazi, alisema hayo jana wakati wa ziara ya moja ya viwanda vilivyo chini ya mamlaka hiyo Kibaha mkoani Pwani.

"Lengo la tathmini hii ni kuboresha kanzi data ya viwanda vya EPZA Tanzania nzima ambavyo ni zaidi ya viwanda mia mbili," alisema.

Taasisi hiyo ina lengo la kutimiza ndoto za kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda, kuongeza fursa za ajira, kuongeza usindikaji wa malighafi za ndani na kuongezea taifa pato la fedha za kigeni.

"Ushahidi unaonesha kuwa sekta ya viwanda ndio chimbuko la maendeleo ya haraka ya nchi mbalimbali na ni mhimili mkuu wa kutegemewa katika kuongeza thamani ya malighafi tulizo nazo, kutoa ajira kwa wananchi na kuongeza mapato ya serikali pamoja na fedha za kigeni na kuongeza na kuboresha sayansi na teknolojia," alisema.

Alisema moja ya jukumu la msingi la sekta ya viwanda ni kuhakikisha tunazalisha bidhaa zenye ubora wa hali ya juu na kuweza kupenya zaidi katika soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC).

Kwa mfano kupitia uzalishaji wa bidhaa kwenye Maeneo Maalum ya Uwekezaji kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa zitakazouzwa nje (EPZ), ni moja ya fursa muhimu sana katika kukuza pato la Taifa na kuongeza fedha za kigeni nchini.

EPZA ndiyo inahamasiha uzalishaji na pia hutoa leseni kwa wawekezaji katika maeneo haya ya EPZ.

Sekta ambazo kwa sasa zinapewa kipaumbele na taasisi hiyo ni zile za usindikaji wa mazao ya kilimo, ngozi, bidhaa za misitu, vigaa vya teknolojia, usindikaji wa madini na bidhaa za vyuma.

Ili kuleta tija na kupima ufanisi wa viwanda vyake, EPZA imeanzisha mfumo mpya ambao utakuwa na taarifa za wawekezaji wake anina ya malighafi ambazo zinatumika ili kuunganisha value chain na wazalishaji wa ndani kwa nia ya kuleta maendeleo.



Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam mapema wiki hii, alipofikishwa kwa kosa la shambulio dhidi ya jirani yake, Lalit Ratilal (hayupo pichani). Kushoto ni mke wake, Sangita Bharat. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Shahidi aeleza mshtakiwa alivyomshambulia jirani

Na Grace Gurisha

FUNDI Seremala, Dominic Mpakani (43) ameileza mahakama mshtakiwa Bharat Nathwan (57), alivyomshambulia jirani yake, Lalit Ratilal, kwa kumpiga kichwa kifuani kisha akadondoka na nakupoteza fahamu.

Pia amedai kulikuwa na ugomvi kati ya mke wa Nathwan, Sangita, na mke wa Ratilal, Kira, ambao walikuwa wakirushiana maneno kwa ukali kwa lugha ya Kihindi huku na baada ya muda kidogo waume zao walifika kwa pamoja na kuingilia ugomvi huo.

Mpakani alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Aaron Lyamuya, wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, alipokuwa akitoa ushahidi dhidi ya washtakiwa hao.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Grace Mwanga, akisaidiana na Wakili Frank Michael, Mpakani alidai kuwa Julai 21, 2023 alikuwa nyumbani kwa Ratilal maeneo ya mtaa wa Mrima katika jengo la Lohana, alimwita kwa ajili ya kuifanyia kazi zinazohusiana na mbao na kazi zingine ndogo ndogo.

Alidai kuwa alifika katika jengo hilo saa 3:00 asubuhi na bosi wake huyo anakaa ghorofa ya tatu na wakati anaendelea na kazi, Sangita alikuwa amesimama kwenye dirisha lake na Kiran alikuwa kwenye mlango wake. Alidai kuwa kila mmoja alianza kuzungumza kwa ukali na kwa jaziba.

"Lakini nilimsikia Sangita akimwambia mke wa Ratilal kwamba uchafu wake apeleke huko ambapo vitu vyote vilikuwa vimewekwa katika eneo la Ratilal na hakuna kitu chochote kilichokuwa katika eneo la Sangita. Baada ya dakika kadhaa sijui walipiga simu au vipi waume zao walikuja kwa wakati mmoja na malumbano yakaendelea kwa wote wanne," alidai Mpakani

Shahidi huyo alidai kuwa wakati malumbano hayo yanaendelea, wote walikuwa wamesimama kwenye mlango wa Ratilal na baada ya muda Nathwan akampiga kichwa RAtilal na akadondoka kisha akapoteza fahamu.

"Wakati Ratilal yuko chini, Nathwan alikuwa akiendelea kumpiga mateke, Kiran akawa anazuia akiwa chini ndipo tukaacha kazi zetu kwenda kuamulia ugomvi, lakini Nathwan alimsukuma mama huyo na kuzamisha kichwa chake ndani ya ndoo ya saruji iliyochanganywa na mchanga," alidai.

Alidai kuwa kuna fundi wa vigae ambaye alikuwa amefanya mchanganyiko huo kwa ajili ya kuweka vigae nyumbani kwa Ratilal. Baada ya kumtoa Nathwan ndipo alipoanza kutoa lugha ya matusi ikiambatana na maneno kwamba atamwonyesha Ratilal kuwa yeye ni nani.

"Tulipomtoa Nathwan, Ratilal alikuwa kama amepoteza fahamu kwa sababu alikuwa hatikisiki, ndipo tukambeba kumsusha ghorofa ya chini tukamfungua vifungo vya shati na kuanza kumfuta futa ndipo akaamka akaitisha simu zake akapiga simu polisi na hospitali.

"Gari la hospitali likafika likamchukua Ratilal na mke wake na polisi wakamchukua Nathwan lakini walinihoji nikatoa maelezo yangu wakaondoka," alidai.

Shahidi mwingine, Dk. Lucia Augustino (52) wa Hospitali ya Mnanzi Mmoja alidai kuwa Julai 21, 2023 alikuwa idara ya dharura chumba namba 20 muda wa mchana alipokea wateja wawili wenye asili ya kiasia walikuwa wamechafuka kuanzia kichwani hadi miguuni na mama alichafuka sana kuliko baba.

Alidai kuwa alianza kumuhudumia mama (Kiran) kwa kumnawisha na maji ya dripu kwa sababu macho yake yalikuwa yanatoa machozi na pia alikuwa akilalamika kwamba ana maumivu makali ya kichwa, hivyo akamwita daktari wa macho ili kumwangalia.

"Daktari alibaini kwamba jicho la upande wa kushoto limepata madhara san. Mgonjwa aliandikiwa rufaa (rufani) kwenda hospitali ya Regency ilkiyoko karibu na hospitali ya Mnazi Mmoja ili kupata matibabu kwak uwa hapo hakuna vifaa vya kufanya uchunguzi. Baada ya hapo tulimrudisha chumba namba 20, akachomwa sindano ya maumivu,"alidai.

Dk Augustino alidai kuwa alimwangalia mwili mzima, alikuwa ana mamumivu kwenye masikio, macho na kichwa ndipo akamwandikia rufani akaondoka na kuanza kumhudumia Ratilal ambaye alikuwa akilalamika kuwa anaumwa sana kichwa, kizunguzungu na anaona maluweluwe.

Alidai kuwa alimchunguza hadi kwenye miguu, alibaini kwamba alikuwa amevimba kichwani upande wa kulia, kifuani na pia magoti yake yalikuwa yamechubuka, hivyo kumwandikia sindano za kupunguza maumivu na vipimo vya CT Scan.

"Licha ya kumchoma sindano ya maumivu, bado alikuwa anajisikia maumivu makali, ndipo naye akaandikiwa rufaa ya kwenda Regency kwa ajili ya uchunguzi zaidi," alidai na kuongeza kuwa baada ya kumaliza kuwapa huduma zote, walienda kufanya vipimo wakamletea ripoti mbili. Lalit alirudisha ripoti ya CT Scan kutoka kitengo cha koo, masikio na macho.

Dk. Augustino alidai kuwa ripoti ya Kiran ilionyesha kuwa kutokana na kemikali aliyopata katika macho alipata ugonjwa wa jicho na ubongo wake umepata mtikisiko, baada ya hapo alijaza fomu ya polisi (PF3).

Alidai kuwa madhara ambayo anaweza kuyapata ni upofu na pia kidonda chake kinachukua muda mefu kupona, si wiki wala mwezi, kwa sababu kinapona taratibu.

Pia alidai kuwa wagonjwa hao walipata maumivu ya nyama laini, tatizo hilo walitibiwa Mnanzi Mmoja, baada ya hapo alijaza taarifa Julai 21,2023.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Machi 12,2024 kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa kwa mashahidi upande wa mashitaka.

Washtakiwa hao ambao ni raia wa Tanzania wanaoishi Mtaa wa Mrima - Kisutu, jengo la Lohana, Dar es Salaam, wanashtakiwa kwa mashtaka manne waliyoyatenda Julai 21,2023.

# Waziri akunwa utendaji serikali mtandao

**Na Lusungu Helela,** IRINGA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, aridhishwa na utendaji kazi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA).

Pamoja na kuridhishwa huko, ameitaka mamlaka kuongeza kasi zaidi katika kusanifu na kutengeneza mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) ili kuiwezesha serikali kutoa huduma kwa umma kwa haraka na ufanisi.

Simbachawene alisema hayo jana mjini hapa alipokuwa akizungumza na watumishi wa eGA Kituo cha Iringa na aliwataka kuhakikisha serikali inaendeshwa kidijitali kwenye kila nyanja kupitia mifumo wanayoisanifu.

Alisema eGA ni taasisi muhimu katika dunia ya sasa na serikali inahitaji mapinduzi ya TEHAMA ili itoe huduma zake kwa wananchi kwa urahisi na kwa haraka

"Dunia inakwenda kasi na teknolojia ni kila kitu kwa sasa, hivyo ni muhimu kwa eGA kufanya utafiti, kubuni na kutengeneza mifumo ya TEHAMA serikalini kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa huduma kwa umma," alisema.

Simbachawene aliongeza kuwa eGA imeweka juhudi kubwa katika kusimamia TEHAMA serikalini na imetengeneza na inaendelea kutengeneza mifumo ya TEHAMA ambayo imewarahisishia wananchi kupata huduma kwa haraka, mahali popote na kwa gharama nafuu na kuchagiza utawala bora. Aidha, Simbachawene aliwataka watumishi hao kuendelea kubuni mifumo ya TEHAMA inayotatua changamoto zilizopo nchini pamoja na kuwa wazalendo kwa maslahi ya taifa.

Pia aliwasisitiza watumishi wa eGA kuhakikisha mifumo inayotengenezwa na iliyopo inakuwa na uwezo wa kuwasiliana ili kuleta ufanisi katika kuwahudumia wananchi.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao, Mhandisi Benedict Ndomba, alimshukuru Waziri Simbachawene kwa kutenga muda wake kutembelea kituo hicho cha Iringa na kuahidi kutekeleza maagizo yote aliyotoa.



Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete (kulia), akizungumza na Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGa) Kituo cha Iringa jana, kabla ya kumkaribisha Waziri wa Wizara hiyo, George Simbachawene (katikati), kuzungumza nao. Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao, Mhandisi Benedict Ndomba.
**PICHA: LUSUNGU HELELA**

# Vijiji 360 vyote Iringa vyapata umeme

**Na Teresia Mhagama,** IRINGA

USAMBAZAJI umeme vijijini mkoani Iringa umefanyika kwa asilimia 100 baada ya vijiji vyote 360 kusambaziwa nishati hiyo kupitia miradi mbalimbali inayotekelezwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

Hayo yalibainika juzi wakati wa ziara ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, mkoani Iringa kwa ajili ya kuwasha umeme na kukagua miundombinu ya nishati hiyo.

Baada ya kuwasha umeme kwenye kijiji cha Mkangwe wilayani Mufindi, Dk. Biteko aliwataka makandarasi wa miradi ya usambazaji umeme vijijini kutekeleza kazi kwa wakati ili kuendana na kasi ya maendeleo huku akiagiza REA kuwachukulia hatua makandarasi wazembe.

Aidha, Dk. Biteko aliwapongeza makandarasi waliofanya kazi ya usambazaji umeme mkoani Iringa, na kufanya vijiji vyote kuwa na umeme kufikia Desemba, mwaka jana.

Akiwa katika kijiji cha Mkangwe, Dk. Biteko alizindua Zahanati ya Kijiji hicho na kuagiza uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi kuhakikisha inaanza kuhudumia wananchi ipasavyo kuanzia keshokutwa baada ya huduma ya umeme kufika kwenye zahanati hiyo na ikijumuisha kuwapo kwa rasilimali watu na vitu.

Katika hatua nyingine, Dk. Biteko aliwataka wananchi wa Iringa bila kujali itikadi zao, kupendana na kushirikiana katika shughuli za kiuchumi na kijamii na kamwe itikadi zao zisiwafanye watengane.

Kuhusu uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika mwaka huu, Dk. Biteko aliwataka wananchi kuchagua viongozi wanaowasikiliza, wanaotambua changamoto zao na jinsi ya kuzitatua. Pia aliwataka wagombea watakaoteuliwa na vyama vyao, kutozungumza lugha za maudhi wakati wa uchaguzi kwa kuwa

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan anataka maridhiano kwenye nchi na si kugawanyika.

Hafla ya uwashaji umeme katika kijiji cha Mkangwe, ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwamo Mkuu wa Mkoa wa Iringa,

Halima Dendego, Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, Mbunge wa Mufindi Kusini, David Kihenzile na Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Innocent Luoga.

# Mlima kuingizwa orodha ya vivutio

**Na Ashton Balaigwa,** SAME

MLIMA Kidenge ulioko Same mkoani Kilimanjaro, unatarajiwa kuingizwa katika orodha ya vivutio vya utalii vilivyoko kwenye wilaya hiyo.

Hatua hiyo imetokana na wawazawa waliotembelea eneo la mlima huo siku ya kwanza ya tamasha la kuibua na kutangaza vivutio vya utalii katika wilaya ya Same linalofahamika kama " Utalii Festival " linalofanyika wilayani hapa.

Katika tamasha hilo, mamia ya watalii kutoka ndani na nje ya wilaya ya Same wametembelea mlima huo wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Abdallah Mwaipaya, na kupanda kilele cha mlima huo unaotajwa kuwa wa kipekee kutokana na mandhari yake.

"Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan, alianza kwa kutuonyesha njia ya nini tunachopaswa kufanya na leo (jana) kupitia wilaya ya Same nimeandika historia kwenye maisha yangu kwa kupanda Mlima Kidenge. Kipindi tunapanda tulikuwa tunasikia joto lakini tulipofika kileleni upepo wa ufukwe wa bahari unasubiri," alisema Mwaipaya.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Kasilda Mgeni, alisema wazo la kuanzisha tamasha hilo kuibua maeneo yenye vivutio ambayo hayajatangazwa ni matokeo ya ziara ya mafunzo waliyofanya baadhi ya wakuu wa wilaya nchini China. Alisema katika ziara hiyo, pamoja na mambo mengine, walijifunza uzoefu wa kinachofanyika nchini humo kuibua vyanzo vya mapato.

"Tulienda kwenye mafunzo China kujifunza mambo mbalimbali ya maendeleo na kujionea wanavyofanya wenzetu. Nikiwa kule kuna sehemu tulipita tukaona mlima unaofanana kabisa na Mlima Kidenge.

Tofauti yake mlima ule ulikuwa wa kutengeneza na huu wa kwetu ni mlima asilia, hivyo nikaona nikirudi jambo la kwanza ni kuangalia uwezekano wa kugeuza mlima huu kuwa fursa," alisema.

Alisema malengo ya tamasha hilo la Same Utalii Festival ni kuibua vivutio ambavyo havijatangazwa kufahamika na, pia kuviendeleza viweze kuwa sehemu ya mapato kwa kuwezesha watalii wakiwamo wazawa na raia wa kigeni kutembelea maeneo hayo ambayo katika wilaya ya Same pekee yako mengi.

Mmoja wa wakazi wa wilaya ya Same aliyeshiriki kupanda mlima huo, Halfani Peter, alisema ni vyema kukafanyika utafiti utakaoshirikisha wakazi kwenye kila eneo kuainisha vivutio vilivyoko kwenye meneo yao, ikizingatiwa mkazo kwenye kuhamasisha watalii unaelekezwa zaidi kwenye maeneo ambayo tayari yanafahamika.





## Misikiti, makanisa yasisitiza kulindwa kwa uwekezaji

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

JUMUIYA ya Amani na Maridhiano Taifa (JMAT), imetoa wito kwa misikiti na makanisa kutumika kusisitiza Watanzania kuilinda amani iliyopo nchini ili kuvutia wawekezaji na kuwa na uchumi imara.

Mratibu wa Jumuiya hiyo, Dk. Festo Kilawe, alitoa rai hiyo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na wajumbe wa jumuiya hiyo Mkoa wa Dodoma kuhusu majukumu na wajibu wao katika kulinda amani ya nchi.

Alisema makanisa pamoja na misikiti inapaswa kuendelea kusisitiza umuhimu wa amani katika taifa ili utulivu uliopo uendelee kudumishwa.

"Amani iliyopo inapaswa kuendelea kudumishwa kwa hali na mali kwani uwepo wa amani kutasaidia kuwa na utulivu ambao utasaidia kuvutia wawekezaji na kufanya kuwa na taifa lenye uchumi imara na kutatua kero za wananchi wake" alisema.

Pia alisema moja ya majukumu ya jumuiya hiyo ni kuhakikisha kuwa inahubiri amani na maridhiano baina ya Watanzania ili kuendeleza mshikamani na umoja ulipo.

"Mnapofanya maamuzi msifanye tuu kwa mitazamo yenu lazima kushirikishana kwani mtakumbuka hapo awali palikuwepo na mgogoro baina ya wakrito na waislamu kuhusu suala la uchinjaji nani achinje na nani asichinje lakini jumuiya hii ilisaidia kuondoa tatizo lile na hadi leo hakuna shida tena kwenye jambo lile," alisema

Kuhusu maadhimisho ya Siku ya Amani na Maridhiano, alisema yamepagwa kufanyika Machi 6, mwaka huu, jijini Mbeya na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema siku hiyo watafanya shughuli mbalimbali za kijamii ikiwemo kuchangia damu ili kuokoa maisha ya wagonjwa na majeruhi wenye uhitaji.

Katibu wa Jumuiya hiyo Mkoa wa Dodoma, Augustino Ndimila, alisema pamoja na kutekeleza majukumu yao bado wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ukosefu wa ofisi ya mkoa.

"Changamoto kubwa tuliyo nayo hivi sasa ni ukosefu wa jengo la ofisi ya mkoa ya Jumuiya lakini pia vitendea kazi pamoja na samani bado ni shida," alisema.

# Bangi yatajwa chanzo watoto kuacha shule

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MATUMIZI ya bangi kwa watoto wa shule za msingi nchini yametajwa kuchangia kwa kiasi kikubwa wanafunzi wengi kuacha masomo na kujiunga na vikundi vya kihalifu ikiwamo 'panya road'.

Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za

Kulevya (DCEA), Aretas Lyimo, alisema hayo juzi jijini hapa wakati akifunga mafunzo ya siku tatu kwa waelimishaji umma kuhusu madhara ya rushwa na dawa za kulevya.

Lyimo alisema utafiti unaonyesha matumzi ya dawa za kuelevya nchini, ikiwamo bangi, yanahusisha pia watoto kuanzia umri wa miaka 10 hadi 12, hivyo kuna haja kwa waelimishaji umma kuwekeza nguvu katika kundi hilo.

"Matumizi ya bangi kwa kiasi kikubwa yanachangia wanafunzi wa shule za msingi nchini kuacha masomo kutokana na wengi wao kuanza kutumia bangi katika umri mdogo akili zao zikiwa bado hazijakomaa hivyo kuwafanya kufanya mambo ya kihalifu ikiwemo ubakaji kwenye jamii.

"Lakini matumizi haya ya bangi yamechangia watoto wengi kuacha shule kujiunga na vikundi vya kihalifu kama Panya road ambavyo vimekuwa vikileta taharuki katika jamii kwa kufanya matukio ya ubakaji na kuvuruga amani," alisema.

Lyimo alisema kutokana na hali hiyo ipo haja kwa waelimishaji umma hao waliopatiwa mafunzo kuwekeza nguvu kwenye utoaji wa elimu kwa wanafunzi wa shule za msingi, sekondari na vyuo.

Alisema kundi hilo la wanafunzi wa shule za msingi, sekondari na vyuo kama litapatiwa elimu na kutambua madhara ya rushwa na dawa za kulevya tutakuwa na taifa lenye utulivu na uchumi imara.

"Rushwa na dawa za kulevya madhara yake yanafanana hivyo basi kama waelimishaji umma mtajikita kwenye utoaji wa elimu kwa umma mtasaidia taifa kuwa na watu wasiojihusisha na rushwa au dawa za kulevya," alisema.

Aidha, matumizi ya dawa za kulevya yanaathari kijamii na kiuchumi kwani yanachangia kuathiri nguvu kazi ya taifa na kuondoa utulivu wa nchi.

"Kama taifa litakuwa halina utulivu hata wawekezaji watashindwa kuja kuwekeza kutokana na matukio ya kiharifu yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevya," alisema.

Naibu Mkurungezi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Neema Mwakalyelye, alisema katika mafunzo hayo ya siku tatu, washiriki wamejifunza mambo mbalimbali ikiwemo tatizo la dawa za kulevya.

"Pia wamejengewa uwezo wa namna ya kupambana na dawa za kulevya na vita ya rushwa kwani biashara ya dawa za kulevya kwa sehemu kubwa inahusisha na rushwa," alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba (kulia), akizungumza na viongozi wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania (TARURA), Wilaya ya Iramba mapema wiki hii, baada ya kukagua ujenzi wa barabara ya Meli-Walla hadi Ntwike inayojengwa kwa thamani ya zaidi ya Sh. milioni 669. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Nigeria yajifunza Tanzania ilivyopunguza vifo vya uzazi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UJUMBE wa serikali ya Nigeria umewasili nchini kujifunza namna Tanzania ilivyopunguza vifo vitokanavyo na uzazi.

Takwimu zinaonyesha mwaka 2015 vifo vya watoto wachanga vilikuwa 556 kati ya vizazi hai 100,000 na kwa sasa idadi hiyo imeshuka na kufikia vifo 104 kwa vizazi hai 100,000.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. John Jingu, aliyasema hayo jana kwenye kikao na wajumbe wa serikali ya Nigeria ulioongozwa na Kamishna wa Afya wa Jimbo la Borno, Prof. Baba Gana, waliokuja kwa lengo la kujifunza njia za kupunguza vifo vya uzazi na mtoto hususan kupitia mfumo wa M-mama.

Dk. Jingu alisema mafanikio ya Tanzania yametokana na bunifu katika kukabiliana na vifo vya mama na mtoto na matokeo yameonekana na kufanya Tanzania kuwa sehemu iliyovutia mataifa mengine kuja kujifunza.

"Wenzetu wamejiuliza tumefanyaje?, tumewaambia hii ni kutokana na uongozi imara wa Rais Samia Suluhu Hassan ambae amekuwa ni kinara katika kuhakikisha afya ya mama na mtoto inalindwa kwa kuwa na miundombinu wezeshi na kufanya kazi kwa ubora kote nchini na kuwa na watumishi wanaofanya kazi kwa weledi," alisema.

Alisema serikali imeweka mkakati wa kuzuia vifo vinavyotokana na uzazi mama na mtoto mchanga na kwamba havikubaliki kwa sababu njia za kuvizuia zipo na zinatekelezeka kwa kuwa na jitihada na ubunifu wa uzazi salama ambao unashirikisha jamii.

"Tanzania tuna mfumo mpya wa uzazi salama ambao kwa sasa uko katika Halmashauri 30 kwenye hatua za majaribio na baadae tutaendelea na awamu ya pili katika Halmashauri 110, lengo likiwa ni kuhakikisha wadau muhimu ambao ni jamii wanashirikishwa kikamilifu," alisema.

Prof. Gana alisema Nigeria bado haijapiga hatua kwenye kuzuia vifo vinavyotokana na uzazi hivyo wamevutiwa na jitihada za serikali ya Tanzania na kuja kujifunza.

"Hakuna sehemu nzuri ya kwenda kujifunza kama kwa ndugu yako hivyo kutokana na hatua kubwa mliyopiga kama taifa la Tanzania kwenye kupunguza vifo vya mama na mtoto ndio maana tumekuja kujifunza na kubadilishana uzoefu. Ni ukweli usio pingika kuwa sisi Nigeria bado hatujapiga hatua, pia ujio wetu huu unakwenda kufungua milango ya mashirikiano ya mataifa haya mawili kwa ukaribu zaidi,"alisema.





# ‘Ukodishaji visiwa kuchochea uchumi’

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Saharif Ali Sharif, amesema lengo la uamuzi wa serikali kutumia rasilimali zilizomo nchini na kwenye bahari ni kuchochea ukuaji wa haraka wa kiuchumi.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Mwanakwerekwe, Ameir Abdallah Ameir.

Mwakilioshi huyo alitaka kujua tathmini ya uwekezaji wa soko la utalii kupitia visiwa vidogo vilivyoko Zanzibar.

Sharif alisema uamuzi huo unatafsiri Sera ya Uchumi wa Buluu kivitendo na kwa kipindi cha miaka mitatu, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imevikodisha visiwa vidogo 15 kati ya zaidi ya 50 vilivyoko Zanzibar na kuvutia mtaji wa Dola za Kimarekani milioni 384.4 sambamba na Dola milioni 26 kama fedha ya utangulizi ya kupatiwa kisiwa husika.

“Mheshimiwa Spika, naomba pia kutoa taarifa kwenye Baraza lako tukufu kwamba hadi kufikia Desemba, 2023 visiwa vitatu tayari vimeshaanza kuendelezwa kwa hatua ya ujenzi,” alisema.

Alivitaja visiwa hivyo ni Pamunda A na B kwa mtaji wa Dola milioni 50, Bawe kwa Dola milioni 30 na Mtangani kwa Dola milioni 15. Alisema visiwa hivyo vyote vina miradi ya hoteli na nyumba zenye hadhi ya makaazi.

Kuhusu tathmini, alisema serikali ilifikia uamuzi wa kuvikodisha baadhi ya visiwa baada ya kuona tija kubwa ya kiutalii inayopatikana kupitia nchi za visiwa katika maeneo tofauti ulimwenguni.

Alisema Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, kupitia Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) ilifanya utafiti mwaka 2022 kwa nchi kama Maldives ambapo ilipokea wastani wa watalii milioni 1.6 mwaka 2022, Singapore watalii milioni 6.3, Mauritius milioni 1.4 na Bali milioni 1.0. Alisema visiwa hivyo vinaingiza watalii kwa wingi kwa mwaka kwa mujibu wa takwimu za kanzidata ya utalii ya Umoja wa Mataifa.

“Nchi zote zilizotajwa hapa zmevikodisha baadhi ya visiwa vyao na kuviwekea mikakati ya kuhakikisha uwekezaji unaofanywa katika maeneo hayo ni wa hadhi ya juu, unaozingatia mazingira na unaoingiza fedha nyingi za kigeni kwa watalii wanaofika na kulala,” alisema.

# SMZ yatetea uamuzi malipo ya pensheni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imesema serikali imeamua kutoa fedha ya pensheni jamii kwa wazee kupitia benki kwa sababu njia hiyo ni salama zaidi kuliko utaratibu wa zamani wa kupewa fedha taslimu.

Hayo yalisema jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani, na Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Anna Athanas Paul, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Viti Maalumu, Shadya Mohamed Suleiman, aliyetaka kujua kwa nini fedha za pensheni jamii zinalipwa kwa njia ya benki ambayo ni usumbufu kwa wazee waliofikisha umri wa miaka 70.

Naibu Waziri huyo alisema serikali imechukua uamuzi huo kwa sababu awali yalikuwapo matukio ya usumbufu mkubwa kwa ulipaji wa pensheni katika vituo vilivyochaguliwa. Alisema matukio hayo yaliyojitokeza wakati mwengine kuwasubiri kwa muda mrefu wafanyakazi wa wizara katika kulipa na wakati mwengine hujitokeza jua kali pamoja na mvua. Kutokana na usumbufu huo, alisema imebainika kwamba njia pekee ya kuwalipa wazee pensheni jamii bila usumbufu ni kutumia benki.

“Mheshimiwa Spika, wizara imechukuwa uamuzi wa kuwalipa wazee pensheni jamii kwa njia ya benki kwa lengo la kuondosha usumbufu uliokuwa ukijitokeza mara kwa mara ikiwamo wazee kupanga foleni katika mazingira tofauti hata wakati wa jua na mvua,” alisema.

Hata hivyo, alisema wizara itahakikisha kasoro zote zinazojitokeza katika malipo ya pensheni jamii kwa wazee yanafanyiwa kazi ili kuona nia njema ya serikali inafikiwa.

Alisema serikali imejipanga kuhakikisha malipo ya pescheni jamii yanaendelea kuboreshwa ikiwamo kuongeza kiwango kutoka Sh. 20,000 hadi Sh. 50,000.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri, hilo ni ongezeko la asilimia 150 ambalo limelenga kuhakikisha wazee wanaishi katika maisha bora kutokana na mchango mkubwa waliotoa katika ujenzi wa taifa na ukombozi wa Zanzibar.

“Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar awamu ya nane itahakikisha malipo ya pensheni jamii yanaendelea kwa njia mbalimbali ikiwamo kufanya maboresho makubwa katika malipo ili kuleta ufanisi mkubwa,” alisema.



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu akikata utepe wakati wa makabidhiano ya vifaa vya uboreshaji wa huduma za afya mkoani Tanga jana, vilivyotolewa na Shirika la Health Promotion Support (THPS), kwa ufadhili wa Marekani vyenye thamani ya sh. milioni 800. Kulia ni Mkurugenzi wa Miradi, Kituo cha Marekani cha Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa (CDC), Dk. George Mgomella. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Waziri ataja sababu kiwanda kupewa mwekezaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda imesema kiwanda cha Makonyo kilichoko Wawi, kisiwani Pemba, kimepewa mwekezaji kampuni ya Spice Island kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na kuleta ufanisi.

Waziri wa Wizara hiyo, Omar Said Shaaban, alisema hayo jana wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Wawi, Bakari Hamad Bakari, aliyetaka kujua maendeleo ya kiwanda hicho.

Shaaban aliwaambia wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba serikali imekitoa kiwanda hicho kwa mwekezaji huyo ili kuongeza uzalishaji na kukidhi mahitaji.

Alisema kiwanda hicho ni pekee Zanzibar ambacho huzalisha mafuta ya aina mbalimbali ya makonyo yanayotokana na bidhaa za karafuu.

Hata hivyo, alisema kiwanda hicho ni cha muda mrefu kikitumia teknolojia ya zamani wakati dunia kwa sasa inapita katika mabadiliko makubwa ya teknolojia ya uzalishaji wa bidhaa.

“Mheshimiwa Spika, kiwanda hiki tumempa mwekezaji kwa ajili ya kufanya mageuzi makubwa ambayo yatakwenda sambamba na mikakati ya uzalishaji wa bidhaa mbalimbali yakiwamo mafuta ya makonyo ya karafuu pamoja na mimea mingine ya mazao ya viungo,” alisema.

Aidha, waziri huyo alisema kipaumbele cha kwanza cha ukarabati wa kiwanda hicho kimepewa kwa ajili ya kuajiri wafanyakazi waliopo sasa ambao tayari wanao uzoefu na ujuzi mkubwa.

Alizitaja faida za kiwanda hicho ni kulipa kodi mwa mwaka Dola za Kimarekani 54,000 pamoja na mwekezaji mpya kupewa majukumu ya kuweka mitambo mipya inayoendana na mahitaji ya sasa.

Waziri alisema mitambo hiyo itakuwa na uwezo wa kuzalisha na kuchakata bidhaa za mafuta zinazotokana na uzalishaji wake.




VERA SIDIKA

UKURASA 14






# NANI WA KULAUMIWA?

NDOA kati ya mrembo mwenye wafuasi wengi mtandaoni, Zari Hassan na mume wake Shakib Cham Lutaaya huenda ikavunjika kutokana na wawili hao sasa kuonekana kuwa na tofauti.

Wanandoa hao walifunga pingu za maisha Oktoba mwaka jana, lakini kwa miezi michache kumejitokeza viashiria vinavyoonyesha wawili hao wana tofauti kubwa.

Vyanzo mbalimbali vinaeleza kwamba mgogoro huo ulianzia baada ya mwanamuziki wa Bongo Fleva, Diamond Platnumz, kuweka video katika ukurasa wake wa Instagram akionekana akitembea na Zari huku wameshikana mikono.

Diamond alijaribu kuzuia hisia za watu kwa kuandika ujumbe ambao ulionekana kujikinga kwa kumuita Zari ni dada yake.

Baada ya siku moja Zari naye alichapisha video hiyo mtandaoni na hapo ndipo uvumi ulizidi kuenea kwamba mrembo huyo ameachana na mume wake.

Baadhi ya watu ambao walishiriki katika machapisho hayo, walisema kwamba kuna kila dalili ya Shakib kutupwa pembeni na Zari.

Hata hivyo, walilaumu Diamond kuwa chanzo kutokana na kuingilia mapenzi ya wanandoa hao, bila kujali hata yeye yuko katika penzi zito na mwanamuziki Zuchu, ambaye ni msanii wake kutoka WCB.

BASI SAWA

## Judy Mamah kama Rose Muhando

MWIMBAJI wa muziki wa Injili kutoka Kenya, Judy Mamah, amejizolea mashabiki lukuki baada ya kufananishwa na Rose Muhando.



Akizungumza na BT mapema wiki hii, Judy amesema hali hiyo ya kufananishwa na Rose Muhando inamfanya aongeze juhudi katika muziki wa kumtumikia Mungu.

"Nashukuru wimbo wangu Sawa unafanya vizuri hapa Kenya, mashabiki wananiita Rose Muhando wa Kenya, nasikia furaha na inanipa deni la kuendelea kumtumikia Mungu kwa nguvu zaidi," amesema Judy Mamah.

Mwimbaji huyo ambaye yupo chini ya meneja Roy Captain, amewapa ahadi mashabiki kuendelea kuwahudumia kupita huduma yake.

## Bien kufanya ziara Ulaya

MSANII kutoka kundi la Sauti sol la nchini Kenya, Bien-Aime Baraza, ametangaza kufanya ziara ya kimuziki katika mataifa ya Ulaya kuanzia Machi mwaka huu.

Ziara hiyo ambayo imepewa jina la "Alusa Why Are You Topless" itawaunganisha wanamuziki wawili wa Afrika Mashariki; Xenia Manasseh wa Kenya na Joshua Baraka wa Uganda.

"Afrika Mashariki inavuma kwa vipaji vinavyoongezeka vya nyimbo za R&B na moja ya malengo yangu imekuwa daima kubeba nchi zetu pamoja nami kila mahali ninapokwenda", Ameandika kupitia ukurasa wake wa Instagram.





## NINI KIMEMKUTA IBRAAH?

WADAU wa muziki wa Bongo Fleva nchini, wameonyesha wasiwasi wao kutokana na kushuka kwa mwanamuziki, Ibraah ambaye anatoka lebo ya Konde Gang.

Ibraah ambaye yuko chini ya Harmonize, anapambana kurudisha nafasi yake kwa kutoa nyimbo mbili miezi michache iliyopita lakini bado hazijafanya vizuri katika majukwaa ya muziki.

Baadhi ya wadau wamemtaka msanii huyo kuangalia upya sababu ya yeye kusuasua katika muziki tofauti na wasanii wenzake waliotambulishwa wakati mmoja ambao wanaendelea kutamba.



## Miss Tanzania atabiri makubwa

MWAKILISHI wa shindano la Miss World kutoka Tanzania, Halima Kopwe, ameahidi kufanya vizuri katika fainali itakayofanyika nchini India Machi 9, mwaka huu.

Kopwe, amesema nafasi ya Tanzania katika shindano hilo linalowashindanisha warembo kutoka nchi mbalimbali duniani limeshuka na hivyo anao wajibu wa nchi kurudisha heshima yake.

Shindano hilo lilitakiwa kufanyika Mei mwaka 2023 katika nchi ya Falme za Kiarabu, lakini lilifutwa na kupelekwa nchini India ambako fainali zake zitafanyika katika jiji la New Dail.

FILAMU

## Sofia mchumba wa siku sita

**Na Adam Fungamwango**

HILI ni fundisho kwa watu wote, vijana na hata watu wazima. Kuna tabia ambayo siku hizi imezuka ambayo inaweza kuwaletea matatizo baadaye mkajuta.

Kijana anaweza akawa ndani ya daladala amekaa kwenye siti, akapanda mtu mzima kuliko yeye, baba au mama, lakini, 'akakauka.'

Wapo wanaoshindwa kutoa msaada mdogo tu kwa wahitaji wa wakati huo ulio ndani ya uwezo wao, wakati mwingine hata kusalimia tu tatizo.

Imeshawahi kuwakuta watu fulani wakajuta mbele ya safari. Unashindwa kumpisha baba, babu, mama au bibi kwenye siti, halafu siku unakwenda kwa mpenzi wako kujitambulisha unakuta ndiye mama, mama au mlezi unayempenda. Na kwa bahati mbaya au nzuri anakumbuka kwamba ulishawahi 'kumkaukia' kwenye situ, au ulimtukana sehemu fulani alipokuomba umsaidie kitu fulani.

Filamu ya 'Sofia', inatukumbusha binadamu kutenda wema muda wote na mahali popote bila kutegemea hisani kwa sababu hakuna anayejua mbele kuna nini. Waswahili wanasema wema hauozi. Maana yake unatenda na ipo siku isiyo na jina, siku ambayo hautegemei ikakulipa.

Imechezwa na Fozia Sharamo, akicheza kama Sofia, Andrew Adayi aliyecheza kama Zuma, Akumu Kimani, yeye alicheza kama Haji, Samuel Gichachi, yeye ni Abu. Filamu hii imechezwa nchini Kenya.

Sofia, ni binti mzuri kutoka kijiji cha Majimbo, anapendwa na wavulana watatu ambao wote wanahitaji kumuona. Wavulana hao ni Zuma, Abu na Haji.

Barua zote zinapokelewa, na wazazi wake wakawapa siku sita watoa barua kutoa majibu ya nani atakubaliwa kumuoa binti yao.

Kumbe wazazi walikuwa wametengeneza mtihani bila yao kujua ili kumpata mshindi mmoja.

Kuna kumsaidia mjamzito kuchota maji kisimani, kumsaidia mzee kuchanja kuni na kumsaidia msichana aliyetaka kubakwa porini. Kwa bahati nzuri kila mmoja alifaulu kimoja.

Wa mwisho ulikuwa ni Sofia kubakwa na watu wasiojulikana porini. Abu na Haji kila moja 'akachomoa' kumuoa mwanamke ambaye amebakwa. Ni Zuma pekee ndiye aliyekuja na kukubali kuwa atamchukua hivyo hivyo. Baadaye wote wakajulishwa kuwa yote hayo yalikuwa ni mtego, na Zuma ndiye aliyeshinda, na atamuoa Sofia.




## KUMBE WANAJIREKEBISHA BWANA

**Na Adam Fungamwango**

MIAKA kadhaa nyuma kulikuwa na makosa mengi yaliyokuwa yakijitokeza kwenye filamu na tamthilia za Kitanzania ambapo awali yalikuwa hayaonekani.

Ilikuwa hivyo kwa sababu bado Watanzania walikuwa na ule ushamba wa filamu hasa mwanzoni mwa miaka ya 2000, hivyo kuona kila kitu kipo sawa.

Lakini baada ya macho kufunguka, baadhi ya watu kuanza kuwa na uelewa kwenye uigizaji, wakaanza kuona baadhi ya makosa ambayo awali hawakubaini.

Ndipo baadhi taratibu wakaanza kuhamia kwenye filamu za, Kihispania, Kikorea, Kifilipino na hata Kinigeria.

Mauzo yakashuka na kuwawa na shutuma nyingi. Lakini sasa waandaaji wa tamthilia wameliona hilo na kuanza kujirekebisha.

Ukijumlisha na kuongezeka kwa teknolojia, kumekuwa na maendeleo mazuri kiasi kwamba sasa huwezi kuyaona yale makosa maarufu ambayo huko nyuma tulikuwa tunayaona.

Mapungufu yaliyo kwenye filamu za Kibongo yalisababisha Watanzania wenyewe kuwa na dhihaka mbalimbali ambazo wanazitoa kuonyesha kutoridhishwa na jinsi wanavyoigiza.

**Kila mlinzi lazima awe 'chale'**

Kulikuwa na kama utamaduni uliojitokeza kwenye filamu zetu ambao sijui nani ameanzisha na waongozaji wa filamu wote wakawa wameukariri. Eti mlinzi wa getini ni lazima awe kama vile zimemruka hivi.

Ukiangalia filamu nyingi za huko nyuma, utakuta walinzi wa getini wanakwenda wasanii wa vichekesho, au watu ambao ni lazima wacheze kama 'chale', huku nguo zao zikiwa kuukuu. Iliboa na kuzifanya sinema zetu kuzoeleka na kutabirika. Sasa wamebadilika.

**Anarudi Ulaya na nguo ile ile**

Mhusika anakwenda Ulaya. Halafu anaonyeshwa anarejea anashuka Uwanja wa Ndege akiwa na nguo hiyo hiyo aliyokwenda nayo miaka mitano iliyopita. Tena siyo nguo tu, ila muonekano ni ule ule. Kiuhalisia haikupaswa kuchukua picha mhusika anasafiri na kurejea siku hiyo hiyo. Ilibidi wakae hata wiki. Abadilishe nguo na muonekano. Hivi ndivyo ilivyokuwa kwenye tamthilia na filamu zetu za zamani. Nadhani tatizo lilikuwa ni bajeti, lakini sasa huwezi kukiona tena.

**Anakumbuka zamani, picha Rais mpya**

Mapungufu mengine yaliyokuwepo wakati huo ni kwamba inawezekana mhusika akawa anakumbuka zamani alivyokuwa kijana au mtoto. Lakini unaweza kukuta picha za ukutani nyumbani kwao au ofisini ni za Rais wa sasa.

Uhalisia hapo unapotea na ulikuwa ni uvivu wa kufiriki kwa waongozaji. Ilibidi watafute picha wa Rais ambaye wao walitaka kuonyesha mwaka huo. Au kama vipi ziondolewe wakati wa uchukuaji picha.

**Gereza, kituo cha polisi vichekesho**

Wakati wenzetu ukikuta mhusika yupo gerezani au kituo cha polisi kuna uhalisia mtupu, tofauti na hapa kwetu. Hili bado hadi leo halijarekebishwa sana

Hii siwalaumu sana kutokana na jinsi tu sanaa yenyewe inavyochukuliwa Bongo. Kwa wenzetu wanaweza kuruhusiwa kuigizia kwenye kituo cha polisi mradi tu masharti yafuatwe. Kwa wenzetu watu binafsi wanajenga vitu kama hivyo kwa ajili ya kukodisha kwa kampuni za uigizaji.

**Jambazi lazima avae koti refu**

Kwa hali ya kawaida kabisa, mtu yeyote muovu huficha uhalisia wake wa moyoni. Kwenye filamu za Kibongo za zamani mtu yeyote muovu hasa jambazi ni lazima avae koti refu jeusi na mawani meusi. lengo siyo baya, kuweka uhalisia. Lakini si kila filamu mhusika anatakiwa ajulikane kuwa mtu mbaya hata kwa muonekano. Hili naona wamelirekebisha kwa kiasi kikubwa.




## Beyonce azindua bidhaa yake

MWANAMUZIKI nyota wa Marekani, Beyonce Knowles, amejiingiza katika tasnia ya urembo baada ya hivi karibuni kuzindua bidhaa yake mpya ya kutunza nywele.

Katika mahojiano yake na Jarida la Essence, Beyonce aliwaambia mashabiki zake kwamba ameamua kuingia katika urembo kwa kuzalisha mafuta ya kutunza nywele yanayoitwa "Cecred," ambayo yana ubora wa kimataifa.

"Nadhani uhusiano wangu wa kijamii, mama na mtoto, baba na mtoto, kwa wanawake weusi ambao daima wanatunza kila mtu na ndivyo itakavyokuwa Cecred, katika utendaji wake wa kazi," amesema Beyonce.



## Khaid hana mpango na Valentine

MWIMBAJI maarufu wa Nigeria, Khaid amefichua kuwa hajawahi kutoa au kupokea zawadi wakati wa sikukuu ya wapendanao.

Akizungumza katika mahojiano na nyota wa Big Brother Naija, Phyna kwenye podikasti yake, Khaid amesema kusherehekea sikukuu ya Valantine, amesema yeye wakati wote ni siku ya mapenzi na kwamba hana haja ya kusherehekea.

"Sijawahi kusherehekea Siku ya Wapendanao kulingana na ukweli kwamba sijawahi kuwa na mtu anayeiadhimisha. Sijawahi kushangaa Siku ya Wapendanao au kupewa chochote," Khaid alianza.

## Chioma anatia huruma

MSANII wa filamu za Nollywood, Chioma Okoli amesema amekuwa miongoni mwa wanawake walionyanyaswa kingono wakati akitafuta ajira.

Akizungumza hivi karibuni, mwigizaji huyo alithibitisha kuwa kama walivyo wanawake wengi, pia yeye amenyanyaswa kijinsia na mwanamume ambaye alimuahidi kumpatia kazi lakini akamfanyia mambo yasiyofaa.

"Ndio, nimepata uzoefu wa kunyanyaswa kingono. Nilijaribu kufanya kazi na mtu wakati fulani uliopita, na akanialika ofisini kwake na akanibaka, "amesema mwigizaji huyo.





## Burna Boy hategeki kirahisi

MWANAMUZIKI nyota kutoka Nigeria, Damini Ebunoluwa Ogulu, maarufu kama Burna Boy, amefichua kwa nini bado hana haraka ya kuingia katika ndoa licha ya kuwa na mafanikio katika maisha.

Burna Boy amezungumza na mashabiki wake moja kwa moja kupitia Instagram amesema Mungu jahamuonyesha mwanamke wa maisha yake na ndio maana bado ypo yupo sana.

Amesema kuna baadhi ya wanawake wamejaribu kutumia

uwong ili kuwa naye kimapenzi, lakini amejaribu kuwagundua na kuwakwepa.

## Vera Sidika hataki ndoa

MPAMBAJI wa video za wanamuziki kutoka Kenya, Vera Sidika amepuuza uvumi kwamba yuko mbioni kuolewa tena.

Akitumia ukurasa wake wa Instagram, mrembo huyo ambaye ni mama wa watoto wawili alidai kuwa ndoa ni mtego na kwamba anapenda huru kwa sasa.

"Kamwe siwezi "kuolewa), ni mtego. Napenda uhuru wangu na nafurahia kupitia nyakati nzuri." amesema.





## Waziri asaidia ujenzi nyumba katibu wa UWT

**Na Steven William,** MUHEZA

NAIBU Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamisi Mwinjuma, maarufu Mwana FA, ametoa mabati 80 na misumari kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya Katibu wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Wilaya Muheza, mkoani Tanga.

Akizungumza baada ya kukabidhi msaada huo, Mwana FA, ambaye pia ni Mbunge wa Muheza, alisema ameguswa na jitihada zinazofanywa na umoja huo, kwa kujenga nyumba ya mtumishi wao.

Mwenyekiti wa UWT Muheza, Theresia Ilet, alimshukuru Naibu Waziri huyo, kwa kuchangia bati hizo, akisema ni msaada mkubwa kwa Umoja wa Wanawake wa Chama cha Mapinduzi, lakini pia kwa wananchi.

Katibu wa UWT wa Wilaya ya Muheza, Asnath Jeremia, alisema umoja huo wanajivunia kuwa na Mbunge huyo kwa sasa, kwa kuwa mchango wake wa vifaa, mawazo ya uhamasishaji wa ujenzi huo, ndio umoja wa kufanikisha jambo hilo.

Alisema ujenzi wa nyumba ya mtumishi unafanyika katika eneo la Genge, Wilayani humo.

Ujenzi huo ulioanza mwaka jana, unategemea michango kutoka kwa wanachama wa umoja huo na Wabunge wa Viti Maalum mkoa wa Tanga na wadau mbalimbali.

# Wanawake watabiriwa kushinda uchaguzi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WANAWAKE vinara wa uhamasishaji wa uchaguzi ujao wa serikali za mitaa, vitongoji na vijiji wa mwaka 2024 katika wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, wametabiri asilimia 85 ya wanawake watakaogombea, wana nafasi ya kuchaguliwa.

Hali hiyo inatokana na wanawake walioonyesha njia, akiwamo Rais Samia Suluhu Hassan, kuwaondolea dhana hiyo ya woga.

Jana katika mjadala wa wazi uliokuwa ukihusu mwanamke na uongozi, fursa ya kufanya uamuzi na uwezo wa kumiliki mali, Jenifa Somi, mkazi wa kata ya Mbokomu, alisema wanawake wameajiandaa kushiriki uchaguzi huo.

Mjadala huo uliitishwa na Shirika la Maendeleo la TUSONGE, linaloendesha mradi wa uchumi katika Wilaya za Siha na Moshi.

Kwa mara ya kwanza, uchaguzi huo kwa mwaka huu nchini, utasimamiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, baada ya Bunge kufanya marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vitongoji na Vijiji na Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2025.

"Uongozi wa mwanamke, hasa kwenye jamii umetuletea mafanikio makubwa kwa sababu kwanza, unapunguza unyanyasaji. Tunaweza kwenda kwa pamoja na maendeleo yanaweza kuwa mengi. Kila mwanamke anapenda maendeleo yarudi kwenye jamii.

"Mimi najiamini kwamba nikigombea uongozi wa kijiji, kitongoji au mtaa naweza kupata asilimia 85 ya kura kwa sababu naona tangu nimepata mafunzo ya TUSONGE. Hapa nilipo mpaka sasa hivi nimefika pazuri," alisema Somi.

Kuhusu suala la uamuzi kwa mwanamke, Somi alisema: "Binafsi kwangu mimi pale nyumbani maamuzi yangu yanasikilizwa kwa asilimia 100. Naweza kukaa nikapanga na kuyaweka mezani tukayajadili, tukashiriki wote na yakatendewa kazi.

"Ninasikilizwa kwa sababu ninaweza kuyatenda. Ninapokuwa na mwanga katika jumuiya yangu inanifanya mimi kuweza kusema neno wakaona nilitenda na likaendelea kuwa zuri. Wanawake tunao uoga wa kudhani nikisema kitu fulani sitasikilizwa, kwa sababu anaona nyuma ndivyo ilivyokuwa hajajielewa."

Mwenyekiti Msaidizi wa Jukwaa la Wanawake katika Kata ya Majengo, Grace Komba, alisema kutokana na kuwa kiongozi kwenye jamii, amewasaidia wanawake mbalimbali kutatua changamoto zao hasa kwenye jamii.

"Niko kwenye Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi, kwa hiyo nawasaidia kawanza wale wanawake kuwapa mawazo mbalimbali kwa sababu tayari wewe ni kiongozi ulipata elimu, unawapa mawazo mbalimbali kwamba wafanye nini na sio wakae tu nyumbani wawe tegemezi kwa wanawaume.

"Sasa hivi na mwaka huu wanawake wengi wamejitolea mwaka 2024 kugombea nafasi mbalimbali katika serikali za mitaa. Hata uchaguzi mkuu ujao wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2025 watu wamejiandaa. Kwa sasa hivi huwezi kusema nitagombea au sitagombea lakini kutokana na elimu niliyopata nawapa na wengine ambao wanajiandaa 2024 kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa," alisema.

Mratibu wa Mradi huo wa Uchumi, Haika Manase, alisema wanawake katika kata hizo, wanajadili kwa pamoja na kushirikishana uzoefu kuhusu suala zima la uongozi.



Kawaida (kushoto), akisalimiana na mchimbaji maarufu wa madini ya Tanzanite, Bilionea Saniniu Laizer, akiwa katika ziara yake wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Dk. Philip Mpango aagiza matumizi sahihi fedha

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

MAKAMU wa Rais Dk. Philip Mpango, ameitaka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (Tanga UWASA), kufanya matumizi sahihi ya fedha za hatifungani kwa ajili ya kutekelezea miradi ya maji ili kujenga imani kwa wadau wake.

Dk. Mpango aliagiza hayo jana, wakati alipokwenda kuzindua hatifungani ya kijani ya Mamlaka hiyo ya Maji.

"Napenda kuwapongeza wakurugenzi wa Bodi na viongozi wengine pamoja na wafanyakazi wa Tanga UWASA kwa uthubutu wa kutufungulia njia hii mbadala ya kupata fedha za kugaramia miradi ya maendeleo.

"Ni imani yangu kuwa, hamtashawishika kuwekeza fedha za hatifungani hii ambayo ina riba ndogo katika fursa nyingine, mkifanya hivyo kuna hatari ya kupoteza imani ya wadau kutumia njia hii, endapo malengo hayatatimia, kwahiyo tujitahidi sana kuzingatia," alisema.

Aidha, kupitia uzinduzi wa hatifungani hiyo, Makamu alitoa maelekezo ya kuzingatia kwa Wizara ya Maji na kusema, hatifungani hiyo iliyozinduliwe iwe chachu ya maendeleo kwa taasisi na halmashauri zingine kutumia njia hii katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

"Kwahiyo ninaielekeza Ofisi ya Msajili wa Hazina, kama msimamizi wa taasisi na mashirika ya umma nchini, lakini pia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, kama msimamizi wa halmashauri,

"Mhakikishe kuwa taasisi, mashirika na baadhi ya almashauri kuhakikisha zinatumia njia hii ili kuharakisha utekelezaji wa miradi na kutoa nafasi kwa serikali kwenye maeneo mengine ya kipaumbele ambako hakuna uwezeshaji wa aina hii," aliagiza.

Pia aliiagiza Bodi ya Wakurugenzi wote wa Tanga UWASA kusimamia vizuri matumizi ya fedha zitakazo patikana kupitia hatifungani hiyo lakini pia mapato mengine mtakayokusanya baada ya kukamilisha mradi.

"Nidhamu ya fedha na usimamizi thabiti ndio utakaowezesha kurejesha kwa wakati fedha za wawekezaji wa hatifungani hii, serikali haitaweza kuvumilia uzembe wa aina yoyote utakaoonekana kukwamisha juhudi za Mheshimiwa Rais," alisema.

Aliongeza kuwa: "Natambua kwamba mamlaka zetu za maji, kwa kiwango kikubwa zinafanya vizuri, lakini niwakumbushe Tanga UWASA, kuongeza ufanisi katika uendeshaji ili urejeshaji wa hatifungani hii usiwe sababu ya kuzorota kwa huduma au ongezeko la bei ya maji hapa Tanga na kwengine ambako tumepanga mradi huu ufike".

Aidha, Dk. Mpango aliziagiza Mamlaka ya Masoko na Mitaji ya Dhamana kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Wizara ya Maji, kuweka utaratibu na mfumo wa tahadhari ili kufuatilia na kubaini mapema vihatarishi vinavyoweza kujitokeza.


"Kwa kuwa urejeshaji wa fedha hizo ni kwa mkupuo baada ya kulipwa kwa hatifungani, inaweza kuleta shida wakati wa malipo, kwahiyo ni vema kujipanga mapema na ikiwezekana kufungua mfuko maalumu na kukusanya kidogo kidogo fedha za marejesho," alisema.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Mgunduzi, Mmarekani mweusi, alivyobuni msosi pendwa chipsi

## -Alianza kwa kususa, walaji wakanogewa
## -Leo hii imetimu miaka 173 zinatamba

**Na Adam Fungamwango**



George Speck, maarufu kama Crum (kushoto), huyu ndiye mgunduzi wa chips duniani.



Chips kavu, ambazo ndizo haswa zilivumbuliwa na bwana Crum, kabla ya baadaye wateja wake kutaka kuchanganyiwa na mayai.

ANGEZALIWA Tanzania angeweza kupewa tuzo na akinadada wa kuanzia miaka 40 kushuka chini.

Angelaumiwa na baadhi ya wanaume ambao kuna wakati mifuko yao inalazimika kutoboka kwa ajili ya kuwanunulia wapenzi wao chakula pendwa kinachoitwa chipsi.

Kinadada zetu akose chakula chochote lakini siyo chipsi. Anaweza kufululiza hata wiki anakula chakula hicho hicho bila kubadilisha na wala haoni tabu, mradi tu kama ana pesa za kukipata, au yupo wa kumnunulia.

Kama ni mpenzi wake ndiyo anayemnunulia, du, ataonekana wa maana sana na mapenzi yatanoga shatashata.

Siku hizi hata baadhi ya vijana nao wameanza kuzihusudu sana, angalau wanaweza kula mchana chakula kizito, lakini jioni wakapata chips.

Au wanaweza kula mchana kwa sababu wapo maofisini, na jioni ndiyo wanakwenda nyumbani kula ugali au wali.

Nathubutu kusema ndiyo chakula pendwa kuliko vyote kwa sasa hapa nchini.

Wali, maharage, wali kuku, sijui biriani, pilau, sawa, lakini vyote haviwezi kufua dafu kwa chips.

Nenda sehemu yoyote wanapouza chakula cha aina nyingine, halafu nenda kwa wauza chips utaona tofauti. Huwezi kuthubutu kuzungumzia mlo wa 'take away', usikute chips.

Sehemu zenye watu wengi utakuta foleni, hutohudumiwa kwa muda unaoutaka wewe.

Utakuta watu wameshaagiza, chips kuku, chips mayai, maarufu kama zege.

Yaani hiyo mayai mabichi yanachanganya na chipsi na kutengeneza kitu hicho cha 'chips zege.'

Simulizi inanoga pale ninapokujulisha rasmi kuwa mgunduzi wa chipsi ni 'mswahili,' kiasi kwamba inajenga kiuliza ni ndugu yetu nini? Mgunduzi wa chakula hiki ni Mbongo nini? Maana Wabongo kwa kupenda chipsi siyo poa.

Inatia shaka na kujiuliza kwa sababu wengi wanapenda chipsi, inawezekana mgunduzi huyu ana unasaba na Tanzania. Haishangazi kukuta watu wanahoji, mioyoni mwao, je mgunduzi huyu babu yake ni mtoto wa Magomeni Dar, pale ya jijini Mwanza, au kule Mwanjelwa Mbeya?

Naam! Si mwingine ila ni George Speck, maarufu kama Crum, Mmarekani mweusi alizaliwa Julai 15, 1824 katika mji wa Saratoga, jijini New York, na akafariki dunia Julai 22, 1914.

Ndiyo! Nikisema Mmarekani mweusi ni watu wenye asili ya Afrika, ambao babu zao walitoka huku na kwenda kuuzwa kama watumwa ughaibuni, ikiwemo nchini Marekani.

Jamaa alikuwa mpishi kwenye mgahawa wake akipika vyakula mbalimbali, na moja aina ya chakula alichokuwa akiwauzia wateja wake ni viazi mbatata.

Siku moja wakamkera wateja wa viazi vya kukaanga wakamkera. Wakamlalamikia kuwa anawakatia mapande makubwa na wao hawana midomo mikubwa na vikiwa vya moto wanaungua sana.

Hii ilimkasirisha sana, George, lakini hakubishana nao ila lake lilikuwa rohoni. Akapanga kuwakomoa wateja wake.

"Wanasema nawakatia mapande makubwa, sasa wataipata freshi." Badala ya kupunguza kwa kutaka vipande vidogo vya kawaida, yeye akaamua kukata vipande vidogo zaidi kuliko kawaida ili kuwakomoa.

Akaanza kuwakatia hivyo na kuwapelekea, akitegemea watalalamika na yeye akajibu kuwa, "si mlisema vipande vikubwa, sasa hangaikeni navyo hivyo."

Wakati anasubiri malalamiko kutoka kwa wateja kuwa vipande vimekuwa vidogo sana ili awachambe, akaona kimya.

Cha ajabu ni wala viazi hao wakachanganyikiwa na aina mpya ya vipande hivyo, kwani vilikuwa vitamu zaidi na vinavyolika kwa urahisi.

Badala ya malalamiko aliyotegemea akaanza kupokea pongezi na kumhusudu mara moja.

Watu wakaanza kuongezeka kwenye mgahawa wake, akipokea wahitaji wengi waliotoka kona mbalimbali kuja kufaidi aina mpya ya viazi vya kukatwakatwa vipande vidogo vidogo, vilivyoanza kuitwa chips.

Wateja walinogewa zaidi, ghafla ikaanza bili mpya, "changanya na mayai." Na hapo ndipo chipsi zilipoanza kuchanganywa na mayai kwa sababu kwa yale mapande aliyokuwa akiyakata mwanzoni isingewezekana.

Chakula hicho maarufu kama 'kiepe', kikavuka boda kila miaka ilivyozidi kusonga mbele na kufika hadi Bongo mwanzoni mwa miaka ya 1990 na wala haina mpango wa kuondoka leo wala kesho.

Nchini Marekani jamaa alipata umaarufu mkubwa na chipsi zikawa zinajulikana kwa jina na 'Saratoga Chips', kumuenzi mgunduzi huyo ambaye amezaliwa kwenye mji huo.

Haya Wabongo, mkiwa mnakula chipsi mkumbuke kuwa aliyegundua hivyo ni bwana Crum kwa bahati mbaya, baada ya kulaumiwa na wateja wake.

**Tuma meseji 0716 350534**



Kibanda: Kibanda cha Chips.

HABARI KIMATAIFA

# Watu 13,088 wakimbia machafuko Msumbiji

**MAPUTO,** MSUMBIJI

UMOJA wa Mataifa umesema wimbi jipya la machafuko katika eneo la Kaskazini mwa Msumbiji, limesababisha maelfu ya watu 13,088 kukimbia makazi yao katika mkoa wa Cabo Delgado.

Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia uhamiaji (IOM) lilisema kuwa mashambulizi yalitokea hivi karibuni katika mikoa ya Macomia, Chiure na Mecufi.

Idadi kubwa ya watu waliokimbia makazi yao ni watoto na wanawake ambao walitumia mabasi, maboti na wengine kutembea kwa miguu kwa ajili ya kukimbilia sehemu salama.

Rais wa Msumbiji, Filipe Nyusi, alithibitisha kuwepo kwa wimbi jipya la watu kukimbia miji iliyoko sehemu hizo kwa kuhofia kushambuliwa na wanamgambo wenye siasa kali.

Akizungumzia kitisho hicho, alisema maofisa wa usalama wameidhibiti hali hiyo. Rais Nyusi alisema watu walionekana wakitoroka kutoka mji wa Ocua wakikimbia mashambulizi ya kulipiziana kisasi baada ya wanajeshi wa Msumbiji na Rwanda kufanikiwa kuvunja jaribio la utekaji nyara wa watoto katika eneo hilo.

Kulingana na msemaji wa shirika la Umoja wa Mataifa la kuwashughulikia wakimbizi (UNHCR) mwezi uliopita kulikuwa makundi ya wanamgambo waliojihami Kusini mwa mji wa Cabo Delgado.

Aliongeza kuwa mashambulizi hayo yaliharibu majengo ya makanisa, nyumba za watu, shule, miundo mbinu na hata taasisi za afya.

**DW**

# Wapalestina 71 wauawa katika shambulizi

**GAZA,** PALESTINA

MAOFISA wa wizara ya Afya ya Ukanda wa Gaza inayosimamiwa na kundi la Hamas wamesema mashambulizi yaliyofanywa jana na vikosi vya Israel yamewaua watu 71 kusini mwa mji huo.

Hayo yameripotiwa wakati kiongozi wa kisiasa wa Hamas, Ismail Haniyeh, aliondoka nchini Misri baada ya kufanya mazungumzo kuhusu uwezekano wa makubaliano ya usitishaji vita kwa ubadilishanaji wa mateka na wafungwa wa Palestina walioko katika magereza ya Israel.

Wanadiplomasia wa Ulaya wamezidisha shinikizo la kutaka mapigano yasitishwe kama tahadhari ya maafa ya kibinadamu yanayozidi kuenea Ukanda wa Gaza.

**DW**

# Marekani yaonya nchi ya Iran

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI imeonya nchi ya Iran kuwa itakabiliwa na majibu makali kutoka jumuiya ya kimataifa ikiwa itapeleka makombora ya balistiki nchini Russia.

Kauli hiyo inatokana na taarifa za shirika la habari la Reuters ambalo lilieleza kuwa Iran ilipeleka aina hizo za silaha nchini Russia.

Msemaji wa Baraza la Usalama la Ikulu ya Marekani, John Kirby, aliwaambia waandishi wa habari juzi kuwa serikali ya nchi hiyo haijapata ushahidi wa kuthibitisha kuhamishwa kwa makombora hayo kutoka Iran hadi Russia.

Shirika la habari la Reuters liliripoti Jumatano, likinukuu vyanzo sita, kwamba Iran ilisafirisha idadi kubwa ya makombora yenye nguvu ya balestiki nchini Russia.

Kirby alisema ripoti ilieleza kwamba Iran ilionyesha wazi kwamba watasafirisha makombora ya balestiki nchini Russia, lakini Marekani haina sababu ya kufikiria kwamba hawatachukua hatua juu ya suala hilo.

"Sisi kwa upande wetu tunalizungumzia suala hili katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Tutaweka vikwazo vipya dhidi ya Iran na tutazingatia chaguzi zaidi kama jibu kwa uratibu wa washirika wetu barani Ulaya na kwingineko duniani." Alisema Kirby

Katika ripoti yake, Reuters ilinukuu vyanzo vitatu vya habari vya nchini Iran kwamba ilipeleka makombora 400 nchini Russia, yakiwemo idadi kubwa ya makombora ya masafa mafupi ya Fateh-110.

Reuters liliandika kuwa, shehena ya silaha hizo ilianza kusafirishwa kuanzia Januari, baada ya makubaliano kukamilika mjini Tehran na Moscow mwishoni mwa mwaka jana. Kirby alisema kuwa Iran imeuza nje idadi kubwa ya ndege zisizo na rubani, mabomu ya kuongozwa na risasi za kivita kwa Russia ambazo ilitumia katika vita nchini Ukraine.

**BBC**



Uharibifu uliofanywa na vikosi vya Israel katika mji wa Rafah hivi karibuni. **PICHA: AP**

# Waasi M23 wajaribu kuteka mji wa Sake

**GOMA,** DRC

WAASI wa M23 walijaribu kuteka eneo la Mayutsa katika mji wa Sake, wakati Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) Felix Thsisekedi, akitoa hotuba kuhusu usalama wa nchi hiyo.

Hata hivyo vikosi vya jeshi la nchi hiyo (FARDC) na wanamgambo Wazalendo wanaoungwa mkono na serikali walizima jaribio hilo kwa kuwarudisha nyuma waasi hao.

Mapigano hayo yaliyotokea juzi usiku na kuendelea hadi jana asubuhi yamesababisha vifo vya watu watatu na wengine wane kujeruhiwa.

Hata hivyo jana kulikuwepo na hali ya utulivu kurejea katika mji wa Sake, ambao bado uko chini ya udhibiti wa jeshi la serikali na wapiganaji wazalendo. Katika hotuba yake kwa taifa, Rais Tshisekedi alirudia kuituhumu nchi ya Rwanda inawasaidia waasi wa M23, na kuongeza kuwa hiyo ndiyo sababu hawezi kuzungumza na kundi hilo.

"Mazungumzo ningependa kufanya na Rwanda kwa sababu wao ndio walionishambulia. Nilimwambia Paul Kagame kule Addis Ababa kwamba ni ninyi niliopenda kuzungumza nanyi na kuwauliza wanapenda nini kwa nchi yangu na watu wangu?" alisema Tshisekedi.

Kiomngozi hiyo aliwahakikishia watu wake kwamba anafanya kila awezalo kutafuta amani mashariki mwa nchi yake.

**DW**

# Rais Senegal atangaza mwisho wa utawala wake

**DAKAR,** SENEGAL

RAIS wa Senegal Macky Sall, amesema ataondoka madarakani wakati muhula wake utakapokamilika Aprili mwaka huu.

Hata hivyo, kiongozi huyo hakusema tarehe kamili ya kufanyika uchaguzi mkuu ambao awali uliahirishwa.

Rais Sall, alisema tarehe ya uchaguzi itategemea mdahalo wa kitaifa uliopangwa kuanza Jumatatu, ambao unajumuisha mashirika ya kiraia, vyama vya kisiasa na wagombea.

"Aprili 2, mwaka huu dhamira yangu kama mkuu wa Senegal utafikia kikomo, ningependa mjadala huu utatuliwe kwa uwazi," alisema akizungumza kupitia televisheni.

Tangazo lake hilo linapunguza hofu kutoka kambi ya upinzani kuwa alikuwa akipanga kuongeza muda wake.

Awali alitangaza kuahirisha uchaguzi hadi Desemba akieleza ili kuhusu kumaliza mizozo ya wagombea ambao walikuwa na mapingamizi.

**DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ROSE PHILIPO MWAKAJILA**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T 320 AGH(CANTER)** jina la kwenye kadi ya Gari ni Emmanuel Pius Mkwama Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi **PHQ/IRI/MUF/1982/2024.**

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE DISTRICT DELEGATED COURT OF MOROGORO**
**AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 3393 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**

**ELIGIUS EDWARD MWOMBELA..............DECEASED**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR A LETTER OF ADMINISTRATIX BY**
**SOPHIA PETER MASANJA..........PETITIONER**
**SUZAN ELIGY MWOMBELA........PETITIONER**

**CITATION**
**(Made under rule 75 of the probate and Administration of Estate rules, CAP 352 R.E 2019)**

ALL person claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 12 day of 3/2024
Dated at Morogoro this 22 day of 2/2024

PRM/SRM/ Resident Magistrate.
Morogoro

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF KILOMBERO**

**DISTRICT AT IFAKARA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 02 OF 2024**

**In the matter of the Estate of the late PROSPER PHIDOLINE LIHANJALA**

**BY PETER PROSPER LIHANJALA**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 05 day of MARCH 2024

Dated at IFAKARA this 22 day FEBRUARY 2024

RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT RESIDENT MAGISTRATE
KILOMBERO - IFAKARA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya GEITA**

**Kituo cha NYANKUMBU Mkoa GEITA**

**Shauri la madai Na 13/2024**

**Jina la Mdai: DAVID CHARLES**

**Jina la Mdaiwa: ELIUD MUGANYIZI**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuniya 18 ya kanun iza taratibu Madai katika mahakama za Mwanzo)**

**Kwa:ELIUD MUGANYIZI**
**WA MKOANI GEITA-0656-623071**

Kwa kuwa mdai ameleta madai ya Fedha Tsh.1,450,000/-.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsikatika mahakama hii tarehe 26 Mwezi 02 Mwaka 2024 saa 8.00 asubuhi .Kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe13 Mwezi 02 Mwaka 2024

HAKIMU
RESIDENT MAGISTRATE
GEITA.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa mirathi Na. 254/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU BAKARI KAMBI WA ..............**

**KATIKA SHAURI KA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA MOHAMMED BAKARI KAMBI**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 5 Mwezi 03 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 22 Mwezi 02 Mwaka 2024

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 2851/ 2024**

**In the matter of the Estate of the late ELIZABETH MABAI ULAYA of Kitenge within Dodoma City**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**

**BY KHERI ALPHANI ULAYA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above- named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 25 Day of 03, 2024

Dated at Dodoma this 22 Day of 02, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 27 LA 2024**

**ANNETH MALIMI ..................MUOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**PROSPER ZACHARIA..................MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**
**PROSPER ZACHARIA**

**POPOTE ULIPO/MLIPO**

**ANNETH MALIMI** Amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni( mwananyama-la). Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 21/03/2024 saa 3:00 Asubuhi mbele ya **Mh. J.W. SILLAS** Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya abraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa baraza hili leo tarehe 22 Mwezi 02 2024

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

---


**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042,**

**DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI,

KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa kwa maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri. Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging. Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile. Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekan kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosababisha kuwa na tundu kichwani. Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# HADITHI

# DAMU YA MARIAMU-1

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

Akaendelea kujitazama kwa mara ya tatu kwenye kioo. Hata yeye mwenyewe alijionea wivu. Akajikubali kuwa ni mzuri.

Kumbe hata wanaume wanavyotukanana, kupigana na hata kutishia kuuana walikuwa sahihi.

"Wana haki, maana si kwa uzuri huu." Akajiambia mwenyewe akiwa anajitazama kwa mara nyingine tena kwenye kioo kikubwa kilicho mbele yake.

Ni mwanamke ambaye kila mwanaume alitamani kuwa naye. Sura yake ya mviringo, rangi yake maji ya kunde, mashavu ambayo yalikuwa na vishimo ambavyo vilijidhihirisha wazi pale anapocheka.

Uzuri wake hapo unaongezeka kwa mwanya, uliojiegemeza kwenye mpangilio mzuri na meno maupe kama theluji.

Pua yake ilikuwa mchongoko, na kushoto kwake kiliota kidoti cheusi ambacho kiliendelea kuupamba urembo wa msichana huyo.

Macho yake meupe ya duara malegevu, yaliwafanya wanaume kuona kama yanawaona hadi ndani ya mioyo yao.

Alikuwa na umbile namba nane, hipsi zilionekana vizuri, na nyuma ya sura yake alikaa vizuri na kuwa kivutio si kwa wanaume tu bali hata kwa wanawake wenzake.

Nao walikuwa wakimuona walikubali kuwa pamoja na kwamba nao ni warembo, lakini mwenzao amependelewa.

Sifa za uzuri wake ziliendelea kutikisa si eneo la Tabata tu analoishi, bali maeneo mengi ya Dar es Salaam.

Umaarufu wake ukaenea hadi kwa watu ambao bado hawajawahi kumtia machoni. Na wale ambao walibahatika kumuona, walikiri kuwa hawakudanganywa.

Ni mwanamke aliyependeza kwa kila mwanaume ambae alibahatika kukutana naye. Atakayepiga miluzi haya. Atakayemsalimia sawa. Na mwingine kumwita kabisa.

Uzuri alionao alirithi kutoka kwa mama yake mzazi. Anakumbuka wakati wa mwanzo wa usichana wake mama yake alimkalisha chini baada ya kuona ameanza kufuatwa na wanaume kama nyuki anavyofuata maua.

Nyuki wanavyopishana kugombea maua kwa ajili ya kutengeneza asali ndiyo ambavyo wanaume wa rika mbalimbali, vijana kwa wazee walivyoanza kummezea mate.




**Na kweli, hadi leo Mariamu siyo mrembo wa kubabaishwa na watu wenye vyeo, pesa, magari, na vinavyofanana na hivyo.**

Akayekumbuka vizuri maneno ya mama yake. Ni miaka 10 imepita tangu ayasikie yakitoka mdomoni mwa mama yake, aliyefariki miaka minne tu iliyopita.

"Mwanangu wewe ni mkubwa sasa umekuwa mkubwa sasa. Sina maana kuwa mkubwa kwa umri, hapata, ila umepevuka. Unaweza kulijua zuri na baya, lakini kiumri lakini bado mdogo sana, huna mengi hujayajua.

Hawa wanaume ambao wameanza kukunyemelea, usidhani wanakufuata kwa sababu anakupenda sana, au wanataka kukusaidia. Nia yao ni kufyonza asali. Nina maana wanaufuata huo uzuri wako.

Mwanangu wewe ni mzuri, umenirithi mimi, na sisi kwenye familia yetu wote tuko hivyo. Lakini huu uzuri ndiyo una shida. Una rangi nzuri, nywele shepu, umetimia binti yangu, ninachoshukuru una tabia nzuri sana, ila usiufanye mwili kuwa ndiyo kitenga uchumi."

Sauti ya mama yake ilimrudia kichwani mwaka wakati huo akiwa amesimama kwenye meza ya mapambo.

Akachukua chupa ya mafuta ya kulainisha nywele, akafungua na kumimina kiasi mkononi, halafu akaupeleka kichwani na yakasambaa kichwani, yeye mwenyewe akihakikisha yanaenea kwenye nywele zake zote ndefu kwa kutumia mikono yake miwili.

Aliporidhika, akashusha tena mkono wake na kuchukua chupa nyingine ndogo kuliko ile ya mwanzo.

Hii ilikuwa na mafuta ya kulainisha ngozi. Alimimina mkononi na kuanza kujipaka. Akaanzia kwenye mapaja yake yaliyonona, laini, yalioonekana yana rangi inayokaribiana na wekundu

"Nakwambia hivyo kwa sababu mimi hapa unavyoniona mama yako, usinione hivi, mimi nilikuwa mzuri na mrembo sana, nimeeka tu sasa." Bado sauti ya mama yake ilizidi kumuandama kichwani.

"Nilikuwa siwezi kutembea mtaa mzima sijasimamishwa na mwanaume. Pikipiki zitasimama, bajaj zinasimama mama wee, gari, hiyo miluzi ndiyo usiseme, ili mradi tu mama heka heka njia nzima."

Akaangua kicheko peke yake ndani. "Mama naye, mmh, alikuwa na maneno. Sijui kwa nini leo nimemkumbuka sana mama yangu." Akacheka na kujiuliza mwenyewe.

"Lakini leo wapi. Nimezeeka. Uzuri siku zote ni wa muda. Hasa sisi wanawake ni kama maua tu, asubuhi tunachanua, jioni tunanyauka. Kwa hiyo mwanangu usibabaishwe na uzuri ulionao. Kuwa mtu na wakaida, usifanye tena wewe kila mwanaume akikusifia unambeba. Watakakumaliza na kukuacha hapo hapo. Akili yako ndiyo itakupatia namna ya kuishi, siyo uzuri. Mimi mama yako ningependa mwanangu usome, au uwe mfanyabiashara, na hicho kiwe ndicho kitu kitakachotegemea kuishi, siyo uzuri wako ukufanye uishi."

Na kweli, hadi leo Mariamu siyo mrembo wa kubabaishwa na watu wenye vyeo, pesa, magari, na vinavyofanana na hivyo.

Angeweza kuwa ana mshefa wa maana amempangia nyumba Masaki, Oysterbay, Mbezi Beach, na sehemu nyingine za ushuani.

Mwenyewe ameamua kuishi maisha ya kawaida tu. Amepanga nyumba ya vyumba viwili na sebule maeneo ya Tabata.

Amesumbuliwa sana na waume wenye hadhi na pesa, lakini wapi. Harubuniki, hababaiki, kwani mwenyewe pamoja na umri wake mdogo tu wa miaka 25, ana maduka yake mawili ya vipodozi, Tabata na Buguruni, saluni ya kike Ilala na ya kiume Mtoni, vitega uchumi ambavyo vinamuingizia pesa zinazomtosha kabisa kuendesha maisha yake na kusaidia hata ndugu zake.

Ana mpenzi mmoja tu. Naye wala si tajiri, hana cheo wala umaarufu wowote. Ni fundi makenika. Watoto wa mjini wanasema fundi gereji. Kazi yake ni kutengeneza magari maeneo ya Buguruni Dar es Salaam.

Kwa sababu nifundi mzuri wa kuaminika, pesa ya kula au kuvaa wala haikumpiga chenga.

Yeye ndiye alikuwa mkuu wa gereji hiyo. Mmiliki alimpa cheo hicho kwa sababu alimletea wateja wengi kutokana na umahiri wa kutengeneza magari.

Anaitwa Kamal. Huyu ndiye aliyekuwa akimiliki chuma hicho. Mrembo, tishio la jiji, Mariamu.

ITAENDELEA JUMAMOSI

# NGOME, UHAMIAJI HAPATOSHI Z'BAR

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

TIMU za Ngome FC na Uhamiaji FC zitakuwa na kazi kubwa ya kusaka pointi tatu muhimu kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Zanzibar zitakapokutana kwenye uwanja wa Mau A, Unguja ukiwa ni mchezo wa mzunguko wa 19 wa ligi hiyo.

Wakati timu hizi zikioneshana kazi Unguja, huko Pemba kwenye uwanja wa Finya, Jamhuri SC itakabiliana na Kipanga FC.

Ngome FC wamekuwa katika wakati mgumu tangu kuanza kwa Ligi kuu ya Zanzibar ikiwa ni msimu wao wa kwanza kucheza Ligi hii baada ya kupanda daraja msimu uliopita.

Timu hiyo inaburuza mkia katika msimamo wa Ligi kuu yenye timu 16 ikiwa na pointi 12 katika michezo 18 iliyocheza mpaka sasa.

Akizungumza na Nipashe, Kocha Mkuu wa timu hiyo Omar Khamis "Matu", alisema matarajio yake ni kuona wanashinda mchezo huo muhimu ambao ametabiri utakuwa mchezo mgumu kwa pande zote.

Alisema kwa upande wao, wanahitaji kupata alama tatu ili kuendelea kupambana kujinusuru kushuka daraja mwishoni mwa msimu huu.

"Ni mchezo muhimu sana, tunajua hatupo kwenye nafasi nzuri, ni mchezo ambao kwetu sisi ushindi ndio matokeo muhimu zaidi kwetu," alisema Khamis.

Aidha, alisema hana kikosi kibaya ambacho kitashindwa kupata matokeo mazuri bali kuna kuzidiana mbinu za kiuchezaji na ujanja wa maamuzi ndani ya mchezo jambo linaloisumbua timu yake.

Alisema bado kuna changamoto kwa baadhi ya wachezaji kushindwa kuwa wabunifu uwanjani lakini pia kuzitambua kwa haraka mbinu za wapinzani wao katika kusaka matokeo.

"Kila mchezo tunaocheza hivi sasa kwetu sisi ni muhimu ili tupate matokeo ya alama tatu kutimiza malengo yetu, tunajua kama michezo yote katika mzunguko huu ina mapambano makali kwakuwa kila timu inataka kutimiza ilichojipangia", alisema Khamis.



Mwalimu wa michezo wa watoto wanaolelewa na Shirikisho la mpira wa miguu Tanzania (TFF), John Memba, akichora chini kuwafundisha watoto hao wakati walipokuwa wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Shule ya Uhuru Mchanganyiko jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wadau 800 kushiriki katika mkutano Utamaduni, Sanaa

Na Shufaa Lyimo

ZAIDI ya wadau 800 wanatarajiwa kushiriki kwenye mkutano wa mwaka wa Utamaduni na Sanaa uliopangwa kufanyika jijini Dar es Salaam Februari 29.

Awali mkutano huo ulipangwa kufanyika Februari 15 lakini ulilazimika kusogezwa mbele kwa sababu ya msiba wa Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowasa.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Mtendaji Mkuu Taasisi ya Serikali ya Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania (TACAF), Nyakaho Mahemba alisema maandalizi yanaendelea vizuri kuelekea kwenye mkutano huo ambapo kwa mwaka huu kauli mbiu yake ni 'Rasimika Unufaike'.

Aidha, aliwataja baadhi ya viongozi watakaoshiriki Mkutano huo kuwa ni Waziri Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo, Dk Damas Ndumbaro, Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Utamaduni na Sanaa, AbdulMajid Nsekela pamoja na Katibu Mkuu Wizara hiyo Gerson Msigwa.

"Maandalizi yanaendelea vizuri kuelekea kwenye mkutano huu wenye lengo la kuwakutanisha wasanii ili wafahamiane na kubadilishana mawazo na wadau kutoka taasisi mbali mbali", alisema Mahemba.

Alisema mkutano huo utawakutanisha wadau wa Utamaduni na Sanaa kutoka Sekta binafsi na umma ili wajenge mtandao wa kufahamiana na kubadilishana mawazo.

Aliwataka wadau mbali mbali kujitokeza kwa wingi kwa kuwa wataweza kufahamu yote ambayo walikuwa hawayafahamu kupitia mkutano huo.

"Siku hiyo kutakuwa na mambo mbali mbali ambayo yatajadiliwa hivyo ni fursa kwa kila mdau kufahamu mambo mbalimbali, waje mapema ili wajifunze wasiyoyajua ili waweze kufanya vizuri katika kazi zao za Utamaduni na Sanaa," alisema Mahemba.

## Kidunda kumlipia kisasi Kiduku kwa Msauzi

Na Saada Akida

BONDIA wa ngumi za kulipwa hapa nchini Selemani Kidunda amesema atapambana kuhakikisha anampiga mpinzani wake Asemahle Wellem raia wa Afrika Kusini ili kumlipia kisasi bondia Twaha Kiduku.

Kiduku alipigwa na bondia huyo kwenye pambano lililofanyika mwaka jana jijini Dar es Salaam.

Kidunda na Wellem wanatarajia kupanda ulingoni Machi Mosi jijini Dar es Salaam kwenye pambano la raundi 12 kuwania mkanda wa WBF.

Akizungumza na Nipashe jana, Kidunda alisema amefanya maandalizi mazuri kwa ajili ya pambano hilo na anahitaji kulipa kisasi baada ya Asemahle kumpiga Kiduku mwaka jana hapa nchini.

Alisema amemsoma mpinzani wake na kuona ubora na madhaifu yake, anaimani kubwa ya kufanya vizuri katika pambano hilo na kuhakikisha anamchapa mpinzani wake mapema.

"Tunatambua kuwa Asemahle alishawahi kuja hapa Tanzania na kufanikiwa kuondoka na Mkanda, safari hii hawezi kuondoka na pointi hapa nyumbani kwa sababu nahitaji mkanda huo lakini nataka kulipa kisasi kwa Mtanzania mwenzangu," alisema Kidunda.

Kabla ya pambano hilo linalosubiriwa kwa amu kubwa na wadau wa ngumi, pia kutakuwepo na mapambano ya utangulizi ambapo Nassib Ramadhani atapigana na Emmanuel Nadjalakutoka Namibia, Hamad Furahisha atapigana na Ally Mwerange, Lupakisyo Shoti atacheza na Jacob Maganga wote kutoka Tanzania.

Aidha, Salim Jengo wa Tanzania atapigana dhidi ya Gray Chimkwapulo kutoka Malawi, Mohammed Hamad kutoka Tanzania atazichapa na Aidin Muzei wa Uganda , Omary Siltan atapigana dhidi ya Salim Athuman na Loren Japhet atapanda ulingoni kuzichapa na Hillary Katuya wa Zambia.



## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**MAGUIRE, CASEMIRO BASI TENA**
KIUNGO wa kati wa Brazil, Casemiro mwenye umri wa miaka 31, mlinzi wa Ufaransa Raphael Varane mwenye miaka 30 na beki wa kati wa England, Harry Maguire mwenye miaka 30, ni miongoni mwa wachezaji 11 ambao wanaweza kuwa sehemu ya wachezaji wa Manchester United watakaofungashiwa virago msimu huu. (ESPN)

**HATIMA YA TEN HAG**
MWEKEZAJI wa Manchester United Sir, Jim Ratcliffe, ambaye ameweka kipaumbele katika kuhakikisha soka la Ligi ya Mabingwa Ulaya ni jambo la kwanza, anataka kusubiri hadi mwisho wa msimu kabla ya kuamua kuhusu mustakabali wa kocha, Erik ten Hag. (*Star*)

**TUCHEL AITAKA MAN**
NAFASI ya kuinoa Manchester United inamvutia Thomas Tuchel, ambaye ataondoka Bayern Munich mwishoni mwa msimu huu. *(Sky Germany)*

**LIVERPOOL ILIKATAA**
LIVERPOOL ilikataa mpango wa Chelsea kumnunua mshambuliaji wao wa Uruguay, Darwin Nunez mwenye umri wa miaka 24 msimu uliopita wa joto. (*Times*)

**ONANA KUTUA ARSENAL**
ARSENAL imedhamiria kumsajili kiungo wa kati wa Ubelgiji na Everton, Amadou Onana mwenye umri wa miaka 22, msimu huu. (*TeamTalks*)

**AMORIM ATAJWA LIVERPOOL**
KOCHA wa Sporting Lisbon, Ruben Amorim anapigiwa upatu kuinoa Liverpool iwapo watakosa kumleta kocha wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso kuchukua nafasi ya Jurgen Klopp msimu ujao. *(Independent)*

**DIER KUBAKI BAYERN**
MLINZI wa Tottenham Hotspur na England, Eric Dier mwenye umri wa miaka 30, huenda akabakia Bayern Munich zaidi ya msimu wa joto huku timu hiyo ya Ujerumani ikiwa na wasiwasi juu ya kiwango chake cha mchezo. (*PPicture via Mail*)

**BOBB MKATABA MPYA**
KLABU ya Manchester City inakaribia kumfunga kwa mkataba mrefu mshambuliaji wa Norway, Oscar Bobb mwenye umri wa miaka 20. (*Mail*)

**HOJBJERG HATABAKI**
KLABU ya Tottenham Hotspur haitarajii kiungo wa kati Pierre-Emile Hojbjerg mwenye umri wa miaka 28, kubakia katika klabu hiyo msimu huu huku timu kadhaa za Serie A zikiwa na nia ya kumnunua mchezaji huyo wa kimataifa wa Denmark. (*Football Insider*)

**SMITH KUNASWA ARSENAL**
ARSENAL inakaribia kumnasa nyota wa Rangers, Alexander Smith mwenye umri wa miaka 15, huku kiungo huyo mkabaji mzaliwa wa Scotland mwenye uraia wa nchi mbili, akiwa ameiwakilisha Marekani chini ya umri wa miaka 15 na timu ya Scotland chini ya umri wa miaka 16. (*Sun*)

**GREGORIO AWINDWA JUVE**
JUVENTUS inamtaka mlinda lango wa Monza, Michele di Gregorio na wanamwona Muitaliano huyo mwenye umri wa miaka 27 kama anayewezekana kuchukua nafasi ya namba moja wao kwa sasa, Wojciech Szczesny, huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland akiwa na umri wa miaka 33. (*La Gazzetta dello Sport*)

**CASEY ATAZAMWA**
BRIGHTON na Celtic ni miongoni mwa klabu kadhaa zinazomtazama mshambuliaji wa Charlton Athletic raia wa Ireland, Patrick Casey, mwenye umri wa miaka 18. (*Football Insider*)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# PEP GUARDIOLA: SASA NAITAKA TIMU YA TAIFA

**MANCHESTER,** England

**Kocha huyo amesema anatamani kuinoa timu ya taifa kwenye mashindano makubwa kabla....**

PEP Guardiola amesema anataka kuinoa timu ya taifa kwenye michuano mikubwa kabla hajastaafu rasmi ukocha.

Guardiola ana mkataba na Manchester City hadi mwaka 2025 na hajakataa kusaini mkataba mpya.

Hapo awali alihusishwa na majukumu ya kuzinoa timu za taifa za Brazil, England na Marekani na akasema angependa kuchukua jukumu la mashindano makubwa, Kombe la Dunia, Ubingwa wa Ulaya au Copa America kabla ya mwisho wa taaluma yake.

Alipoulizwa na ESPN Brasil ni nini kimebakia kwake kufikia mafanikio ya ukocha, Guardiola alijibu: "Timu ya taifa. Ningependa kufundisha timu ya taifa kwa ajili ya Kombe la Dunia au michuano ya Ulaya. Ningependa hilo."

Alipoulizwa kama anapendelea nchi gani kuiongoza, kocha huyo mwenye umri wa miaka 53 alisema: "Sijui ni nani atanitaka! Kufanya kazi kwa timu ya taifa lazima wakutake kama klabu."

Guardiola tayari ameshinda mataji nchini Hispania, Ujerumani na England na kubeba Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tatu.

Ameziongoza kwa nyakati tofauti Barcelona, Bayern Munich na Man City ambapo kwa pamoja ameshinda jumla ya mataji 32 makubwa, lakini alisema hajajiwekea lengo la kuongeza Kombe la Dunia, Euro au Copa América.

"Sijawahi kufikiria hivyo, kushinda Kombe la Dunia," alisema.

"Nilipoanza katika hili sikuwahi kufikiria kushinda taji la ligi au kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya. Hapana. Nilifikiria, nina kazi? Sawa.

"Ningependa kuwa na uzoefu wa kuishi kupitia Kombe la Dunia, au Euro au Copa América, au chochote kile. Ningependa hilo.

"Sijui itakuwa lini, ikiwa ni miaka mitano, 10, 15 kutoka sasa lakini ningependa kuwa na uzoefu wa kuwa kocha kwenye Kombe la Dunia."

# ALONSO HANA JIBU KUHUSU LIVERPOOL, BAYERN MUNICH



**MUNICH,** Ujerumani

XABI Alonso amekataa kuzungumzia uvumi unaoendelea kumuhusisha na nafasi zijazo za majira ya joto katika klabu za Liverpool na Bayern Munich.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 42 amekuwa mmoja wa makocha wanaoinukia barani Ulaya tangu achukue mikoba ya Leverkusen mwishoni mwa 2022.

Liverpool na Bayern zimeonesha nia ya kuitaka huduma yake wakati klabu zote mbili zitakuwa hazina makocha mwishoni mwa msimu huu.

"Labda una maswali kuhusu mustakabali wangu. Sina jipya la kusema kuhusu hilo. Nilitaka kusema hivyo mapema. Sasa hivi, mimi ndiye kocha hapa, hilo ni la uhakika.

"Kwa siku zijazo sina jipya la kusema, tutaona," alisema Alonso alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari nchini Ujerumani kwa mara ya kwanza tangu Bayern itangaze kwamba Thomas Tuchel ataondoka katika klabu hiyo mwishoni mwa msimu.

Wakati kipaumbele cha Liverpool ni uteuzi wa Mkurugenzi mpya wa michezo baada ya kuondoka kwa mwajiri wa muda mfupi, Jorg Schmadtke mwishoni mwa Januari, Alonso yuko kwenye orodha fupi ambayo tayari imeundwa na uongozi wa Anfield pamoja na Roberto De Zerbi na Ange Postecoglou.

Kwa mujibu wa ripoti, Bayern ilimtazama Alonso, ambaye aliwakilisha klabu hiyo mwishoni mwa maisha yake ya uchezaji, hata kabla ya kuamua kujiondoa kwenye utawala mfupi wa Tuchel huko Bavaria.

Alonso bila shaka angekuwa chaguo maarufu kwa mashabiki wa Liverpool. Alishinda taji la Ligi ya Mabingwa ambalo halikutarajiwa katika msimu wake wa kwanza kama mchezaji na mwanawe alizaliwa Liverpool.

Lakini Alonso ana uhusiano wa wazi na Ujerumani pia, licha ya maisha yake ya zamani na Bayern, kuhamia Munich kutoka Leverkusen bila shaka kungekuwa na msukosuko mdogo kuliko kurejea England.

Leverkusen wamejipatia jina la utani la kikatili 'Neverkusen' kwa miaka mingi kutokana na uwezo wao wa kuanguka kwenye kizingiti cha mwisho, kama inavyothibitishwa na washindi wa pili katika Bundesliga mara tano katika kipindi cha miaka 30 iliyopita bila kushinda.

Msimu wa 2001/02 ulikuwa wa uchungu sana katika suala hilo, na kizazi cha Leverkusen kilikuwa na nafasi ya tatu, na kumaliza katika nafasi ya pili kwenye Bundesliga na kupoteza fainali ya DFB Pokal na fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na kumaliza kampeni bila chochote.

Alonso atakuwa na matumaini ya kuachana na alama hiyo, akiwa na uongozi wa pointi nane zikiwa zimesalia mechi 12 kwenye msimamo wa sasa wa Laligi dhidi ya Bayern, ambao wameshinda kila taji tangu 2012.

## Kroos atangaza kurejea kikosi cha Ujerumani

**MUNICH,** Ujerumani

TONI Kroos atarejea katika timu ya taifa ya Ujerumani kabla ya michuano ya Ulaya msimu huu wa joto, kiungo huyo wa kati wa Real Madrid alithibitisha kwenye mtandao wa kijamii jana.

Kroos mwenye umri wa miaka 34 ambaye alistaafu soka ya kimataifa mwaka 2021 alikuwa amefichua mapema mwezi huu kwamba alifikiria mpango huo kabla ya Euro 2024, ambayo itaandaliwa na Ujerumani.

"Jamani, kwa ufupi, nitaichezea tena Ujerumani kuanzia Machi," aliandika Kroos kwenye ukurasa wake wa Instagram.

"Kwa nini? Kwa sababu niliulizwa na kocha wa taifa, niko tayari na nina uhakika kwamba mengi zaidi yanawezekana na timu kwenye michuano ya Ulaya kuliko watu wengi wanavyoamini!"

Kroos aliichezea Ujerumani mechi 106 kati ya 2010 na 2021, akifunga mabao 17, na alikuwa kiungo muhimu wa timu iliyoshinda Kombe la Dunia la 2014 huko Brazil.

Alistaafu baada ya kukosolewa kwa uchezaji wake kwenye Euro 2020, Ujerumani ilipotolewa na England katika hatua ya 16 bora.

Kiungo huyo amekuwa kwenye maisha bora zaidi kwa kikosi cha Real Madrid msimu huu, na kuisaidia kuongoza msimamo wa LaLiga.



# Alves ahukumiwa miaka minne jela



**KATALUNYA,** Hispania

MAHAKAMA Kuu ya Katalunya imemkuta na hatia na kumhukumu kifungo cha miaka minne na nusu jela, nyota wa zamani wa Brazil, Dani Alves kwa makosa ya kumnyanyasa kingono mwanamke katika klabu ya usiku jijini Barcelona mwaka 2022.

Mahakama pia iliamuru kwamba Alves alipe fidia ya euro 150,000 kwa mwathirika huyo.

"Hukumu hiyo inazingatia kwamba imethibitishwa kuwa mwathiriwa hakukubali, na kwamba kuna ushahidi, pamoja na ushuhuda wa mlalamikaji, kuzingatia ubakaji uliothibitishwa," mahakama ilisema katika taarifa yake.

Alves mchezaji wa zamani wa Barcelona alishikilia kuwa ngono hiyo ilikuwa ya makubaliano na mawakili wake waliwaambia waandishi wa habari nje ya mahakama kwamba wanakusudia kukata rufaa dhidi ya hukumu hiyo.

Hata hivyo, Alves ataweza kuomba likizo kwa muda mfupi kutoka katika gereza lililo karibu na Barcelona ambako anazuiliwa mara baada ya kutumikia robo ya kifungo hicho na kutimiza matakwa mengine, afisa wa mahakama alisema.

Mahakama ilisema kwamba pamoja na ushuhuda wa mwathiriwa, ilizingatiwa kama ushahidi kwamba aliumia goti baada ya Alves kumsukuma hadi sakafuni.

"Tumeridhika kwani hukumu inatambua kile ambacho tumekuwa tukisema muda wote: kwamba mwathiriwa alikuwa akisema ukweli na kwamba aliteseka," alisema David Saenz, mmoja wa timu ya wanasheria wa mwathiriwa, akiwaambia waandishi wa habari, na kuongeza kuwa timu itachambua kama hukumu inalingana na uzito wa uhalifu.

Wakili wa Alves, Inés Guardiola, hakukubaliana na hukumu hiyo, akisema: "Tutakata rufaa. Bado ninaamini kuwa Dani Alves hana hatia. Bado hatujasoma hukumu yote kwa sababu ni ndefu sana, lakini tutasoma kwa undani sasa. Tunatetea kutokuwa na hatia kwa Alves."

Mwendesha mashtaka aliomba Alves ahukumiwe kifungo cha miaka tisa jela na mwathiriwa aliomba miaka 12, lakini mahakama iliamua miaka minne na nusu, ikisema kwamba aliamua kumlipa mwathirika fidia bila kujali matokeo ya kesi.

HABARI MICHEZO

## Simba yaanza kuunda kikosi cha msimu ujao

INATOKA UK 24

tumeangalia mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu, tumeongea naye, yeye pia anataka kuichezea Simba," kilisema chanzo chetu ndani ya klabu hiyo.

Tchekei, raia wa Togo, anayecheza nafasi ya kiungo mkabaji anatajwa kusajiliwa kwenda kuongea nguvu kwenye eneo hilo lakini pia kusaidia kupiga pasi za mwisho na kusaidia jukumu hilo Clatous Chama ambaye aanatajwa kuwa bora kwenye eneo hilo.

"Tuna Chama, lakini kama hayupo nani mwingine, kama kuna watu waliwaambia anaondoka wamedanganywa, Chama yupo ataongeza mkataba na tunamuongeza Tchakei, ni mchezaji mzuri na sifa nyingine aliyonayo ni ile ile ya kwamba amezoea soka la Tanzania," kilisema chanzo hiko.

Simba ina mpango wa kukifumua kikosi chake ambacho kinaonekana kina wachezaji wengi ambao wamechoka, baadhi wana umri mkubwa ili kutegemeza kikosi chenye wachezaji wengi wapya, vijana, wenye kasi kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

## *Gamondi: Ni mechi muhimu kushinda*

INATOKA UK 24

wachezaji wenzake, beki wa Yanga, Dickson Job alisema kama wachezaji wako tayari kwa asilimia 100 kwa mchezo huo na kazi imebaki kwao wachezaji kuhakikisha wanaondoka na ushindi.

"Tumejiandaa vizuri na tuko tayari kwa ajili ya kutafuta ushindi, morali ipo juu sana jambo la kwanza tumefanikiwa kutinga hatua ya makundi, na sasa tunaiwaza robo fainali, tutapambana sana kupata ushindi," alisema Job.

Kocha Mkuu wa CR Belouizdad, Marcos Paquette alisema anafurahi kufika Tanzania kwa mara ya kwanza na anafahamu Yanga ni timu nzuri hivyo anaamini utakuwa mchezo mzuri.

"Tumejiandaa vizuri, nitawakosa wachezaji wangu watatu ambao ni m ajeruhi lakini nina mbadala wao ambao wanauwezo mzuri na watatusaidia kufikia malengo yetu kwenye mchezo wa kesho (leo).

Tunaifahamua Yanga ina wachezaji wazuri, lina benchi la ufundi zuri ni timu iliyokuwa bora na inaleta ushindani, wanacheza vizuri lakini mipango yetu ni kufuzu kucheza robo fainali," alisema Marcos.

# YANGA YAIPIKU SIMBA KUSHINDA MECHI MFULULIZO LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

VINARA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga inaongoza kwa kushinda michezo mingi mfululizo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara inayoendelea. Kwa mujibu wa dawati la takwimu la Nipashe, timu hiyo imeshinda mechi saba mfululizo wakiwapiku watani zao, Simba ambao wanashika nafasi ya pili kwa kushinda mechi sita mfululizo.

Yanga ilianza kushinda mechi mfululizo kwenye raundi ya tano, mara tu baada ya kutoka kupokea kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Ihefu, Oktoba 4 mwaka jana.

Baada ya hapo ikaanza kutoa dozi kwa Geita Gold ya mabao 3-0, Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza, Oktoba 7 mwaka jana, pia ikaitandika Azam FC mabao 3-2, Oktoba 23 kwenye Uwanja wa Banjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Oktoba 27 ikatoa kipigo cha mabao 2-0 kwa Singida Fountain Gate kabla ya Novemba 5 kushusha kupigo cha mabao 5-1 kwa Simba kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa.

Mechi yake ya tano iliyochezwa Novemba 8, iliiadhibu Coastal Union bao 1-0 kwenye Uwanja wa Mkwakwani, Tanga na Desemba 16 ikaitandika Mtibwa Sugar mabao 4-1 na baadae Desemba 23 ikiilaza Tabora United bao 1-0 kwenye mchezo uliochezwa Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Simba yenyewe ilianza mechi yake ya kwanza ya ufunguzi wa Ligi Kuu msimu huu, Agosti 17 mwaka jana iliporarua Mtibwa Sugar mabao 4-2, Uwanja wa Manungu Complex,Morogoro, na mechi ya pili ikaiadhibu Dodoma Jiji mabao 2-0, Agosti 20 kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, kabla ya kuibamiza Coastal Union mabao 3-0 katika uwanja huo huo Septemba 21.

Oktoba 5 mwaka jana ilikwenda ugenini, Uwanja wa Sokoine Mbeya na kuwachapa wenyeji, Prisons mabao 3-1, kabla ya kwenda mkoani Singida na kutoakipigo cha mabao 2-1 mbele ya Singida Fountain Gate Oktoba 8 na kurejea Dar es Salaam kutoa kipigo cha mabao 2-1 kwa Ihefu FC, Oktoba 28.



Vijana wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam kama walivyokutwa na mpiga picha jana.

# Tanzania Prisons yaipania Azam FC

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha Tanzania Prisons kiko kwenye mazoezi makali kujiandaa mchezo wao wa Ligi kuu dhidi ya Azam FC kesho Jumapili huku ikipania kuondoka na pointi zote tatu.

Tanzania Prisons watawakaribisha Azam kesho kwenye uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo Shaaban Mtupa alisema ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Singida Fountain Gate walioupata Alhamisi iliyopita umewapa chachu ya kufanya vizuri kwenye mchezo huo wa kesho. Alisema wapinzani wao wanapaswa kujiandaa kwa kuwa watakutana na jioni ndefu siku hiyo.

"Tunaendelea na maandalizi kuelekea mchezo wetu na Azam, vijana wapo katika hali nzuri, kila mmoja ana morali, kuna mapungufu ambayo yalionekana lakini tumejitahidi kuyarekebisha na vijana wameshika maelekezo yetu.

"Najua tunakwenda kucheza na timu kubwa, nzuri ambayo imewekeza kwenye usajili na ni moja ya timu chache kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inacheza kimbinu, tumeifuatilia kwenye baadhi ya mechi zake na tumeyafanyia kazi mapungufu yao, tunategemea matokeo mazuri kupitia kwa wachezaji wetu ambao tunawaamini, ukichukulia tumetoka kuifunga Singida mabao 3-1, bado wachezaji wetu wana morali," alisema Mtupa, mshambuliaji wa zamani wa timu hiyo.

Kuelekea kwenye mchezo huo, mshambuliaji wa timu hiyo, Tariq Simba, amesema ni matokeo ya ushindi tu dhidi ya Azam ndiyo yatakayowaweka pazuri kwenye msimamo wa ligi kuzisaka nafasi nne za juu ambazo zinatoa uhakika wa kucheza michuano ya kimataifa msimu ujao.

Prisons iko nafasi ya saba kwenye msimamo Ligi Kuu ikiwa na pointi 20, huku Azam ambayo mechi iliyopita ililazimishwa suluhu dhidi ya Tabora United, Jumatatu iliyopita, Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Tabora ikiwa kwenye nafasi ya pili na pointi zake 36.

Michezo
Nipashe
Jumamosi Februari 24, 2024



Guardiola: Sasa naitaka timu ya taifa UK. 21

# Gamondi: Ni mechi muhimu kushinda

## ●●● Ametaka wachezaji wake kutumia vizuri kila nafasi watakayoipata kwa kuwa...

**Na Saada Akida**

KOCHA wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema mchezo wa leo wa Ligi ya Mabingwa Afrika kundi D ni muhimu zaidi kwa kushinda ili kujiweka katika nafasi nzuri kwenye kundi lao huku akiwataka wachezaji wake kutumia vizuri nafasi watakazozipata.

Yanga leo inacheza na CR Belouizdad kwenye mchezo wa marudiano hatua ya makundi ya michuano hiyo.

**Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Gamondi amesema kuwa ni lazima kuwa makini na nafasi wa takazozitengeneza kwa kuwa mechi kubwa kama ya leo sio rahisi kutengen eza nafasi nyingi kutokana na ubora wa wapinzani wao.**

"Hii ni mechi muhimu sana, kama tunataka kusonga mbele lazima tuangazie matokeo mazuri kwetu, ninaimani hili litawezekana kutokana na maandalizi yetu, kikubwa lazima tutumie vizuri kila nafasi tutakayoipata, mechi kama hizi hazitengenezwi nafasi nyingi" alisema Gamondi.

Mechi hiyo itaanza kuchezwa saa 1:00 usiku, huku Yanga ikihitaji zaidi pointi tatu ili kujiwekea mazingira mazuri ya kusonga mbele kwenye robo fainali ya michuano hiyo mikubwa zaidi kwa ngazi ya vilabu Afrika.

Timu hizo zinakutana huku kila mmoja akiwa na pointi tano, lakini Yanga itakuwa na kumbukumbu mbaya ya kufungwa mabao 3-0 katika mechi ya kwanza iliyochezwa Novemba 24 mwaka jana nchini Algeria.

Yanga kwenye mchezo wa leo itamkosa mchezaji wake mmoja, Zawadi Mauya aliyepata jeraha la mguu katika mchezo wa kombe la FA dhidi ya Polisi Tanzania kwenye uwanja wa Azam Complex.

Gamondi alisema licha ya kupata muda mfupi wa kuandaa timu bado wamefanya maandalizi mazuri kwa ajili ya kutafuta ushindi ambao utaleta furaha kwa mashabiki wa timu hiyo.

"Tulipoteza mechi iliyopita, hiyo imebaki historia, tumesahihisha makosa yetu na kujiandaa vizuri kwa mchezo wetu wa kesho (kesho), tutakuwa makini kila sehemu.

"Tumecheza mechi nne, kesho (leo) tunaenda kucheza mechi ya tano, kwanza tumejipanga kisaikolijia haitakuwa mechi rahisi, lakini tunacheza mbele ya mashabiki wetu hivyo lazima tupambane tupate pointi tatu," alisema Gamondi.

Alisema katika mchezo wa leo watacheza soka la kushambulia zaidi huku wakiwa makini kuziba nafasi kila watakapopoteza mpira.

"Hatutajilinda muda wote bali tushambulia, tunafahamu timu za Algeria zinavyocheza, wajilinda sana wakiwa ugenini huku wakitegemea mashambulizi ya kushtukiza, tumejipanga," alisema.

Akiwazungumzia wapinzani wao, Gamondi alisema CR Belouizdad ni timu nzuri na wametoka kupata sare kwenye mchezo wao dhidi ya Al Ahly hivyo watakuwa na morali kubwa.

Akizungumza kwa niaba ya

INAENDELEA UK 23



Gamondi

# Simba SC yaanza kuunda kikosi cha msimu ujao

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kukiwa na taarifa ya kutaka kumchukua mshambuliaji Fiston Mayele kwa mkopo kutoka Pyramids ya Misri, Uongozi wa Simba umeanza mchakato wa kukitengeneza kikosi imara cha msimu ujao kwa kuwinda wachezaji kadhaa wa ndani na nje ya nchi.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema kuwa mbali na Mayele, klabu hiyo iko kwenye mazungumzo na mchezaji wa Ihefu, Marouf Tchakei ambaye ameonekana kuwavutia mabosi wa Simba, huku pia Feisal Salum akitajwa.

Chanzo kimoja kutoka ndani ya klabu hiyo kinasema viongozi wa klabu hiyo wako kwenye harakati ya kutaka kumtwaa Feisal ili kutengeneza eneo la kiungo, lakini mchakato wake bado ni mrefu, huku dili la Tchakei likiwa limefika mahala pazuri.

"Mpango wetu msimu ujao ni kutengeneza kikosi imara, lakini pia tumekaa kama viongozi tumeona ipo haja ya kusajili baadhi ya wachezaji ambao wanaifahamu vyema ligi ya Tanzania, ni kweli tumepeleka ofa Misri kumtaka Mayele, na moja ya sababu mbali na kuwa ni mshambuliaji mzuri lakini anafahamu mazingira na soka la Tanzania, hivyo hatutaka tumpe muda.

Vile vike kuna huyu mchezaji aliyekuwa Singida Fountain Gate, anaitwa Tchakei, tulimkosa kidogo tu kipindi cha dirisha dogo, lakini

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042